# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA UCHUMI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**FEBRUARI, 2023**

YALIYOMO UKURASA


1. UTANGULIZI 3

2. OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO 6

3. AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI 23

4. WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI 39

5. HITIMISHO 71

RIPOTI YA KAMATI YA UCHUMI YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

## SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Uchumi ni miongoni mwa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi iliyoundwa kwa mujibu Kanuni ya 107, Jadweli la Kwanza la Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020. Kamati hiyo imepangiwa kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;
ii. Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadiri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji Bajeti na Hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;
iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na ya Wananchi ya Wizara husika;
iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;
v. Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya Wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka;
vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika;
vii. Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufatilia utekelezaji wa ahadi hizo;
viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika;

Katika kutekeleza majukumu yaliyopo hapo juu, Kamati ya Uchumi inasimamia utekelezaji wa shughuli za Wizara tatu zifuatazo:

- Afisi ya Rais, Fedha na Mipango

- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi imeundwa na Wajumbe sita wafuatao:

1. Mhe. Sabiha Filfil Thani - Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Soud Nahoda Hassan - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hassan Hamad Omar - Mjumbe
4. Mhe. Panya Ali Abdalla - Mjumbe
5. Mhe. Rukia Omar Ramadhan - Mjumbe
6. Mhe. Ameir Abdalla Ameir - Mjumbe

Aidha, Kamati ina makatibu wawili ambao ni:

1. Ndg. Nouman Thabit Nouman - Katibu
2. Ndg. Asma Ali Kassim - Katibu

## 1.2 UTARATIBU WA KAZI ZA KAMATI

Katika utekelezaji wa majukumu yake yaliyoainishwa na Jadweli la Kwanza la Kanuni ya 107 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, Kamati ilifanya kazi kwa utaratibu wa kupokea taarifa tofauti za kila robo mwaka (quarterly reports) za utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Wizara, kupokea taarifa za utekelezaji wa Maagizo ya Kamati, kukutana na wadau mbali mbali wa sekta zinazosimamiwa na Kamati pamoja na kukagua baadhi ya maeneo na miradi mbali mbali inayosimamiwa na Wizara zinazohusika ili kuona hatua za utekelezaji zilizofikiwa, changamoto zilizopo na kutoa maoni, maagizo na ushauri wa kutatua changamoto hizo.

Kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilifanya kazi kwa mizunguko minne kwa Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

1. Mzunguko wa kwanza ulianzia tarehe 28 Machi hadi tarehe 01 Aprili 2022 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 04 Aprili hadi tarehe 08 Aprili 2022 kwa upande wa Unguja.
2. Mzunguko wa pili ulianzia tarehe 08 Agosti 2022 hadi tarehe 13 Agosti 2022 Tanzania Bara na kuanzia tarehe 15 Agosti hadi tarehe 19 Agosti 2022 kwa upande wa Unguja.
3. Mzunguko wa tatu ulianza tarehe 24 Oktoba 2022 hadi tarehe 28 Oktoba2022 kwa upande wa Pemba na kwa upande wa Unguja Kamati ilianza tarehe 31 Oktoba 2022 hadi tarehe 04 Novemba 2022.
4. Mzunguko wa nne ulianza tarehe 23 – 27 Januari, 2023 Pemba na tarehe 30 Januari – 3 Febuari 2023 Unguja.

# SEHEMU YA PILI

## OFISI YA RAIS, FEDHA NA MIPANGO

## 2. UTANGULIZI

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango imeundwa na mafungu makuu sita ambayo ni Ofisi ya Rais Fedha na Mipango (F01), Mfuko Mkuu wa Serikali (F02), Tume ya Mipango (F03), Mtakwimu Mkuu wa Serikali (F04), Mhasibu Mkuu wa Serikali (F05) na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Hesabu za Serikali (F06).Mafungu hayo yameundwa na Idara ishirini na tatu (23), Taasisi saba (07) zinazojitegemea na ofisi tano (05) za Pemba.

### 2.1 UKUSANYAJI MAPATO HADI DISEMBA 2022

Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango inasimamia na kukusanya mapato ya aina mbili ambayo ni Mapato ya kodi yanayokusanywa na Taasisi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa upande wa Zanzibar na mapato yasiyokuwa ya kodi yanayokusanywa na Mafungu ya F01, F04 na F05.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2022, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imekusanya jumla ya shilingi 635.662 bilioni sawa na asilimia 101 ya makadirio ya kukusanya TZS 631.048 bilioni.

### 2.2 MATUMIZI JULAI HADI DISEMBA 2022

Kwa upande wa matumizi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2022; imetumia jumla ya shilingi 122.888 bilioni Sawa na asilimia 85 ya makadirio ya shilingi 145.080 bilioni katika kipindi hicho cha mapitio. Kati ya fedha hizo, shilingi 89.621 bilioni zilitumika kwa ajili ya matumizi ya Mfuko Mkuu, shilingi 10.176 bilioni zimetumika kwa ajili ya Mishahara; shilingi 6.950 bilioni kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa mafungu ya OR-FM; shilingi 14.229 bilioni ni Ruzuku zilizopatiwa Taasisi kupitia OR-FM na shilingi 786.354 milioni zimetumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutoka kwa wahisani na shilingi 1.124 bilioni kutoka kwa SMZ.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Mfumo wa utoaji taarifa kati ya Wizara na Taasisi zake unapaswa kuimarishwa ili kuzipa fursa taasisi hizo kufanya kazi kwa ufanisi.
2. Umakini unahitajika kwenye uandaaji wa Ripoti zinazowasilishwa mbele ya Kamati kwani mapungufu yanayojitokeza yanaweza kuipa Kamati taarifa isiyo sahihi na hivyo kupelekea kutoa maagizo yasiyo sahihi pia.
3. Ni wajibu wa Wizara kuishirikisha Kamati kwenye shughuli zake ikiwa ni pamoja na mafunzo, ufunguzi na uzinduzi wa miradi mbali mbali.

## 2.3 MIRADI YA MAENDELEO

### a) MRADI WA USIMAMIZI WA UPEMBUZI YAKINIFU WA PROGRAMU NA MIRADI

Mradi huu umeandaliwa kwa lengo la kuimarisha uandaaji wa ripoti za upembuzi yakinifu kwa program na miradi ya maendeleo nchini na kurahisisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutoa taarifa za kitaalamu zinazoainisha hali halisi ya uwezekano wa utekelezaji wa mradi huo na mbinu za utekelezaji wake kwa ufanisi wa mradi husika. Kwa awamu ya kwanza, mradi unategemewa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (2022/23 – 2024/25) na kugharimu jumla ya shilingi 23.4 bilioni. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, mradi umepangiwa kutumia jumla ya shilingi 6.98 bilioni.

### b) MRADI WA KUIMARISHA USIMAMIZI, KUJENGA UWEZO NA KUOANISHA MIPANGO YA KISEKTA, KITAIFA NA KIMATAIFA

Ni mradi ulioanzishwa kwa nia ya kuimarisha usimamizi na kuoanisha mipango ya kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa. Mipango hiyo inajumuisha mpango wa maendeleo wa Zanzibar (ZADEP), Malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) na Malengo ya maendeleo Afrika (African agenda2063). Kwa mwaka wa fedha 2022/23, mradi umepangiwa kutumia jumla ya shilingi 530 milioni (300 milioni kutoka SMZ na 230 milioni kutoka kwa washirika wa maendeleo).

### c) PROGRAMU YA UKUZAJI UCHUMI JUMUISHI ZANZIBAR BIG – Z

Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar ina lengo la kuimarisha hali ya maisha na kukuza Maendeleoya kiuchumi katika maeneo yaliyoteuliwa ya Zanzibar katika utoaji wahuduma, uhifadhi wa urithi na usimamizi jumuishi wa Miji. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi huu umekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 47.13 bilioni.
Hadi kufikia Disemba 2022, mradi umetumia jumla ya shilingi 571.5 milioni sawa na asilimia 1.21 ya makadirio ya shilingi 47.13 bilioni.

Miongoni mwa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo ni:

Kupatiwa mafunzo wafanyakazi na wadau wa mradi ambapo wafanyakazi na wadau 25 wa mradi wa BIG Z walipatiwa mafunzo ya masuala ya mazingira na mambo ya kijamii katika utekelezaji wa mradi.
Mradi unaendelea kufanya zabuni mbalimbali ili kupata wataalamu na taasisi kutoa huduma za kitaalamu na kusambaza vifaa vitakavyotumika kuendeshea mradi kwa ufanisi. Zabuni zenyewe zikiwemo Zabuni ya Kuajiri Mtaalamu wa Kimazingira na wa Masuala ya Kijamii, Zabuni ya kuajiri Taasisi ya Kusimamia Mradi na Zabuni ya Kuajiri Mtaalamu wa Kuandaa Mpango wa Uendelezaji wa Mji Mkongwe na Michenzani.

### d) PROGRAMU YA UJENZI WA OFISI ZA SERIKALI

Programu hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya kazi ili kuimarisha ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa wananchi. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 programu hii imepanga kutumia kiasi cha shilingi 92 bilioni kwa ujenzi wa Ofisi za Serikali. Kwa kipindi cha Julai – Disemba 2022, Jumla ya shilingi 817.184 Milioni sawa na asilimia 1 zimetumika kwa ajili ya kumlipa Mshauri elekezi wa ujenzi wa Mahakama kuu ya Tunguu. Sambamba na hayo, ofisi zinazokuwemo kwenye Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali zimeanza hatua za awali ikiwemo kazi za kuandaa michoro na upimaji wa maeneo ya ujenzi.

## CHANGAMOTO ZA MIRADI NA PROGRAMU ZA MAENDELEO

1. Upatikanaji wa fedha za miradi hii kutoka kwa washirika wa maendeleo umekua wa kusuasua jambo ambalo nimepelekea kuzorota kwa miradi hiyo.
2. Baadhi ya taasisi za Serikali huwa ni nzito wa kupokea mifumo na kuifanyia kazi jambo ambalo linarejesha nyuma juhudi za Serikali kuu.
3. Uchelewaji wa programu ya Ujenzi wa Taasisi za Serikali unapelekea taasisi mbali mbali kuendelea kutekeleza majukumu yao katika hali ngumu ya uhaba wa nafasi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa ajili ya matumizi bora ya mifumo iliyoanzishwa, Wizara inapaswa kufanya mafunzo kwa wadau wote wanaotakiwa kutumia mfumo huo katika shughuli zao za kila siku.
2. Kutokana na uchelewaji mkubwa wa fedha za miradi ya maendeleo nchini, Kamati inaishauri Afisi ya Rais Fedha na Mipango kutafuta mbinu mbadala za kupata fedha za kuendesha miradi hiyo kwa wakati.
3. Iko haja kwa Serikali kufanya tathmini ya miradi ya maendeleo inayatekelezwa chini ya washirika wa maendeleo na kubaini tija inayopatikana kutokana na miradi hiyo. Aidha, Kamati ya Uchumi inashauri Serikali kuandaa mpango maalum wa kuendeleza manufaa ya miradi hiyo mara baada ya kumaliza muda wa utekelezaji wake.

## 2.4 SHIRIKA LA BIMA LA ZANZIBAR

Shirika la Bima la Zanzibar ni shirika la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar lililoanzishwa mwaka 1969 na linaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009 na Sheria ya Msajili wa Hazina Namba 6 ya mwaka 2021. Ni shirika lililosajiliwa na Kamishna wa Bima Tanzania kutoa huduma za bima katika mfumo wa bima ulioanzishwa mwaka 1998 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shirika hili lilianzishwa kwa lengo la kutoa huduma bora za bima kwa wananchi na taasisi za Serikali na kuwakinga dhidi ya majanga mbali mbali.

Shirika lina jumla ya watendaji 121, mawakala na madalali wa bima 177 na linafanya kazi zake kupitia Makao Makuu yaliyopo Mpirani Zanzibar, Kanda ya Pwani Dar-es-salaam, Kanda ya ziwa Mwanza, Kanda ya kati Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Kanda ya Kaskazini Arusha, Kanda ya Kusini Mtwara, Ofisi ya Mauzo Pemba, Ofisi ya mauzo Tanga, Ofisi ya mauzo Kahama na Ofisi ya Mauzo Posta Dar-es-salaam.

Kamati iliarifiwa kuwa Shirika lina Majukumu makuu yafuatayo:

a) Kusimamia mapato ya Shirika kutokana na vyanzo mbalimbali vikiwemo bima za gari, bima za moto, bima za meli pamoja na mapato yanayotokana na uwekezaji.
b) Kusimami fedha za Shirika kupitia utekelezaji wa bajeti yake inayopitishwa kwa kila mwaka wa fedha.
c) Kusimamia maendeleo ya sekta ya Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau wote.
d) Kusimamia mali za shirika kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za shirika kwa mujibu wa sheria.
e) Kusimamia teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kupitia mifumo inayohusisha kudhibiti mapato na matumizi ya shirika.

Shirika linamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 na limefanya uwekezaji katika maeneo mbali mbali. Kwa mwaka wa fedha 2022, Shirika limefanikiwa kupata faida ya uwekezaji ya jumla ya shilingi 1.05 bilioni kutokana na maeneo yafuatayo:

a) Jumla ya shilingi 2.9 bilioni zimewekezwa kwenye makampuni mbalimbali kwa ununuzi wa hisa kama inavyooneshwa kwenye jadweli lifuatalo:

| JINA LA KAMPUNI | IDADI YA HISA | BEI YA HISA | THAMANI YA HISA |
|---|---|---|---|
| TAN-REE | 23,928 | 1,569 | 37,531,068 |
| ZEP-REE | 134,404 | 16,366 | 2,199,655,864 |
| MWANI | 11.53% | - | 450,000,000 |
| ZAFICO | 10% | - | 261,000,000 |
| JUMLA | | | 2,948,186,932 |

b) Dhamana za akiba kwenye benki (security deposit) zenye jumla ya shilingi 9.2 bilioni katika mfumo wa amana za muda mrefu (fixed deposit) na bondi kama inavyooneshwa kwenye jadweli lifuatalo:

| AINA YA UWEKEZAJI | THAMANI HALISI |
|---|---|
| Akiba za amana za muda mrefu (FDR) | 6,308,000,000 |
| Bondi | 2,450,000,000 |
| Mifuko ya Umoja (MUTUAL FUNDS) | 500,000,000 |
| JUMLA | 9,258,000,000 |

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022, Shirika lilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 44.3 bilioni kutoka katika vyanzo vyake vya mapato na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 38.2 bilioni sawa na asilimia 86% ya makadirio.

Kwa mwaka wa fedha 2022, Shirika limefanya matumizi kama ifuatavyo:

a) Gharama za uendeshaji wa ofisi (management expenses) zenye jumla ya shilingi 8.5 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 89% ya makadirio.
b) Malipo ya madai ya wateja waliopata ajali yenye jumla ya shilingi 4.3 bilioni.
c) Ujira kwa mawakala na madalali wa bima wa jumla ya shilingi 3.3 bilioni

**Kwa upande wa Kanda ya Kusini Mtwara,** Ofisi inahudumia mikoa ya Mtwara, Lindi na Ruvuma na ina jumla ya wafanyakazi wanne na mawakala saba. Aidha, huduma za ofisi

hii pia zinapatikana kupitia mfumo wa (banc assurance) kwa kushirikiana na benki za NMB, CRDB, Exim bank, BOA, NBC na VODA bima.

### 2.4.1 MAPATO NA MATUMIZI

Ofisi ya shirika la Bima kanda ya Kusini inaendelea na jukumu lake la msingi la kutoa huduma za bima kwa wateja na kukusanya mapato kutokana na vyanzo vyake vyengine. Hadi kufikia Julai 2022, ofisi imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi TZS 489 milioni sawa na asilimia 85 ya makadirio.

| | Makadirio kwa mwaka 2022 | Makadirio Jan – Julai 2022 | Mapato Halisi Jan – Julai 2022 |
|---|---|---|---|
| Bima ya Gari | 934,589,208 | 521,369,557 | 420,559,645 |
| Bima ya moto | 60,000,000 | 35,000,000 | 57,066,985 |
| Bima ya meli/ndege | 10,000,000 | 5,800,000 | - |
| Bima mchanganyiko | 30,000,000 | 17,000,000 | 11,684,428 |
| JUMLA | 1,034,589,208 | 579,369,557 | 489,311,058 |

Kwa upande wa matumizi, hadi kufikia Julai 2022, Ofisi imetumia jumla ya shilingi 99 milioni kwa shughuli za uendeshaji, sawa na asilimia 69 ya makadirio kwa kipindi hicho. Matumizi hayo yalijumuisha malipo ya madai halali ya jumla ya shilingi 25 milioni kutoka kwa wateja walioathirika na majanga mbalimbali ya ajali na malipo ya jumla ya shilingi 13.6 milioni kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara ya kuuza bima kwa niaba ya shirika.

### CHANGAMOTO

1. Kupanda kwa gawio kutoka asilimia 20 hadi asilimia 50 kwa faida inayopatikana kila mwaka kutokana na agizo la Serikali kutakakolifanya Shirika kushindwa kukuza mtaji wake.
2. Ofisi ya Kanda ya Kusini Mtwara inatumia jengo la kukodi ambalo linaongeza gharama za uendeshaji na kupunguza faida.

3. Shirika kulazimika kufuata miongozo ya Serikali kama Idara nyengine za Serikali ni jambo linalolibana Shirika kwenda sambamba na ushindani katika soko la bima nchini.
4. Kushindwa kutekeleza mashauri ya Msimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) ambayo yanalitaka Shirika la Bima la Zanzinzibar kuongeza mtaji wake.
5. Adhabu ndogo kwa makosa ya kutokata bima za vyombo vya moto nchini kutokana na kupitwa na wakati kwa Sheria ya Motor Vehicles (Third party risks) Cap 136 ya mwaka 1953.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Shirika lianzishe biashara mpya pamoja na kuwaenzi wateja wa awali ili kwenda sambamba na ushindani wa biashara ya bima nchini.
2. Ili kwenda sambamba na sheria ya Bima Namba 10 ya mwaka 2009, Kamati inashauri taasisi zetu za ZIC na PBZ kutafuta jengo la pamoja kupitia jina la PBZ. Kufanya hivyo kutapunguza gharama za uendeshaji wa mashirika yetu na kuondoa usumbufu unaoyakabili mashirika pamoja na wateja wake.
3. Kamati inaiomba Serikali kulipatia Shirika la Bima la Zanzibar retension kwa kiwango kinachostahiki ili kuongeza mtaji wake na kujiendesha kwa ufanisi zaidi.
4. Kamati inaitaka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kuharakisha marekebisho ya Sheria ya Motor Vehicles (Third party risks) Cap 136 ya mwaka 1953 ili tuwe na viwango vya adhabu vinavyokwenda na wakati na kupunguza makosa ya kutokuwa na bima za vyombo vya barabarani.
5. Ukaguzi wa mara kwa mara unahitajika katika matawi na vituo vya kutolea huduma kwa wateja vilivyopo kwenye kanda mbalimbali nchini ili kuhakikisha kwamba mifumo ya utoaji huduma iko salama na biashara iendelee kwa kasi inayotakiwa.
6. Kamati inashauri Shirika kujitangaza kupitia njia za kisasa ili kuwafikia wateja wengi zaidi.

## 2.5 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Ni benki ya Serikali iliyoanzishwa mwaka 1966 kwa mujibu wa Sheria ya makampuni (Zanzibar Companies Decree, cap 153) na inatekeleza majukumu yake chini ya sheria ya makampuni nambari 15 ya mwaka 2013. Benki hii inamilikiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa asilimia 100. Hadi kufikia tarehe 31/12/2022, PBZ ilikuwa na wafanyakazi 489 kati ya hao wanaume 270 na wanawake 219. Aidha, benki ina jumla ya matawi 18, matawi 10 ya kutolea huduma za kawaida (convensional) na matawi 8 ya huduma za Kiislamu, Vituo 10 vya kutolea huduma, mashine 43 za kutolea fedha (ATM), maduka 7 ya kubadilishia fedha na mawakala 715 katika mikoa mbalimbali ya Tanzania.

Benki imefungua matawi yake katika mikoa tofauti ya Tanzania Bara katika juhudi zake za kutanua wigo wa biashara na kukuza faida. Matawi hayo yanatoa huduma katika mifumo ya aina mbili; mfumo unaofuata misingi ya sheria ya kiislamu (Islamic banking system) na mfumo wa kawaida wa kibenki (conventional banking system).

**Kwa upande wa Mtwara,** Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) ina matawi mawili yaliyopo katika jengo la Posta Mtwara. Matawi hayo yalianza kutoa huduma zake tarehe 30 Agosti, 2016. Aidha, benki ya watu wa Zanzibar imefungua kituo cha kutolea huduma Wilayani Tandahimba ambacho kimo kwenye jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba na kimeanza kutoa huduma kwa wateja tarehe 24 Januari 2022. Kwa pamoja, matawi yote mawili na kituo cha huduma vina jumla ya watendaji 19.

Kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa huduma za kibenki kwa wateja, PBZ Mtwara ina jumla ya mashine mbili za kutolea fedha (ATM) (moja ipo Mtwara mjini na moja ipo Tandahimba). Kadhalika, benki ina mikataba na mawakala 35 waliotawanyika katika maeneo mbali mbali ya Lindi na Mtwara. Mawakala hao wanatoa huduma chini ya mikataba maalum.

Hadi kufikia Juni 2022 (wakati Kamati ilipotembelea), matawi ya PBZ Mtwara yameweza kutoa mikopo kwa wafanyakazi 812 yenye jumla ya shilingi 10.51 bilioni. Aidha, matawi hayo yametengeneza faida ya jumla ya shilingi 3.6 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 124% ya kiwango kilichokadiriwa. Kwa upande wa matumizi, PBZ imetumia jumla ya shilingi 623,714,251.77 milioni kwa kilpindi hicho.

## CHANGAMOTO

1. Ushindani mkali wa biashara dhidi ya soko dogo la Mtwara katika sekta ya mabenki ambapo takribani benki 7 zimeweka matawi yake.
2. Uelewa mdogo wa wakulima na wafanya biashara wadogo wadogo juu ya umuhimu wa kutunza fedha zao benki.
3. Uelewa mdogo wa wateja juu ya umuhimu wa kutumia huduma mbalimbali zinazotolewa na benki kama vile ATM na huduma za benki ya kiislam.
4. Upungufu wa wafanyakazi wa muda ambao wangetumika moja kwa moja kwenye suala la kutafuta wateja wapya na kuongeza amana.
5. Uwepo wa dormant account nyingi kutokana na wateja wa benki kutoa fedha zao zote mara tu baada ya kupokea malipo yao na kutoendelea kutumia akaunti hizo.
6. Benki kutokuwa na mikopo ya kilimo ambayo ni mahitaji ya wakulima wadogo wadogo wa Mtwara.
7. Kutokea kwa hitilafu za kimtandao mara kwa mara kunakosababisha usumbufu mkubwa kwa mawakala na wateja wao.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na ukuaji wa shughuli za Benki ya watu wa Zanzibar (PBZ) Mtwara, Kamati inashauri kuongezwa kwa wahudumu (teller) ili kutoa huduma kwa urahisi katika msimu wa zao la korosho ambapo benki huzidiwa na wateja.
2. Benki ni sehemu ya biashara. Hivyo basi mwonekano wa Benki ya watu wa Zanzibar matawi ya Mtwara uboreshwe ili uwe na mvuto kwa wateja wapya.
3. Kutokana na changamoto ya uhaba wa nafasi kwa matawi ya PBZ Mtwara, Kamati inaitaka Wizara kulishughulikia kwa karibu eneo ambalo linatarajiwa kujengwa matawi hayo na kukamilisha taratibu zote kwa ajili ya kulipata na kufanya ujenzi huo.
4. Ili kumudu ushindani wa sekta ya mabenki katika kanda ya Mtwara na kwengineko nchini, Viongozi na watendaji wanatakiwa kuwa imara na wachangamkie fursa zinapotokea.

5. Kamati inashauri Afisi ya Rais ya Rais Fedha na Mipango kuipatia PBZ Mtwara watendaji zaidi pamoja na vyombo vya usafiri ili kuwafikia wateja katika maeneo mengi.

## 2.6 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Mamlaka ya Mapato Zanzibar imeundwa kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, 2022. Awali mamlaka hiyo ilijulikana kama Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) iliyoanzishwa rasmi Septemba 1998 chini ya sheria Namba 7 ya mwaka 1996 ikiwa na dhima kuu ya kukusanya mapato ya ndani kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Sambamba na hilo, Mamlaka inawajibu wa kumshauri Waziri anaehusika na masuala ya fedha kuhusu maswala ya sera za fedha na kodi.

Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) imepewa uwakala wa kusimamia na kukusanya ada na kodi zilizokua zinasimamiwa na Taasisi nyengine nchini kama ada za leseni ya udereva, leseni za njia, usajili wa vyombo vya moto pamoja na kodi ya ardhi.

Kwa upande wa **Mkoa wa Kaskazini Unguja**, ZRA imetanua huduma zake kwa kufungua ofisi mbili.Ofisi ya kwanza ni Makao Makuu ya Ofisi kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini. Ofisi hiyo imeanza kazi rasmi Julai, 2022 na inatekeleza majukumu yote ya Taasisi yanayotekelezwa na Makao makuu yakiwemo kukusanya ritani za walipakodi, kufanya ufuatiliaji wa kodi, kusajili walipakodi wapya, kutoa leseni za vyombo vya barabarani na kufanya malipo kwa huduma mbalimbali zinazotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

ZRA inaendesha kituo cha huduma kwa wateja kilichopo katika kijiji cha Nungwi katika Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kamati imeshuhudia watendaji wa kituo hicho wakiwa katika hali mbaya ya joto na kukosa vifaa muhimu vya kufanyia kazi vikiwemo kompyuta na genereta.

Aidha, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) inatoa huduma zote kwenye kituo chake kilichopo Michenzani Mall ambacho kimefunguliwa kwa ajili ya kupunguza msongamano wa wateja kwenye ofisi za ZRA Makao makuu na kuwapunguzia usumbufu wananchi.

### 2.6.1 UKUSANYAJI WA MAPATO

Hadi kufikia Disemba 2022, ZRA imekusanya jumla ya shilingi 286.093 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 99 ya makadidirio ya TZS 290.048 bilioni ya kipindi cha miezi sita ya mwaka wa fedha wa 2022/2023. Aidha, makusanyo hayo ni sawa na asilimia 49.36 ya Makadirio ya mwaka kwa kulinganisha na makusanyo ya kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 kuna ongezeko la TZS 115.924 bilioni sawa na ukuaji wa asilimia 68.12.

Ongezeko hili pamoja na mambo mengine, limechangiwa na kuendelea vizuri kwa ukuaji wa uchumi na ongezeko la wageni walioingia nchini ikiwemo na jitihada za uimarishaji wa upokeaji na uchambuzi wa ritani za walipakodi za kila mwezi. Aidha, Ukuaji huu wa mapato ni mkubwa kulinganisha na kasi ya ukuaji wa pato la taifa 6.6 % katika kipindi cha nusu ya mwanzo ya mwaka 2022.

### CHANGAMOTO

1. Uelewa mdogo wa wanajamii juu ya uwepo wa vituo vya huduma kwa wateja wa ZRA pamoja na huduma zinazotolewa na vituo hivyo.
2. Uhaba wa watendaji wa vituo hivyo kwa msimu wa wateja wengi (kati ya tarehe 15-20 ya kila mwezi).
3. Uhaba wa vitendea kazi kama Kompyuta na printa kwa ajili ya kuwahudumia wateja wa vituo hivyo.
4. Mazingira duni ya kituo cha ZRA Nungwi yanawapa wakati mgumu watendaji na wateja wanaofika kupatiwa huduma.
5. Kukosekana kwa jengo maalum la kituo cha huduma kwa wateja Nungwi ambapo Kamati imeshuhudia Jengo linalotumiwa na Kituo hicho ni la Serikali kuu na halina haiba ya kiofisi.
6. Wafanyabiashara wengi wa maduka ya kitalii yaliyopo Nungwi na maeneo mengine hawatowi risiti za kielektroniki wanapofanya mauzo yao jambo ambalo linaikosesha mapato Serikali.

7. Muitikio mdogo wa wafanyabiashara kulipa kodi kwa hiyari unaopunguza makusanyo ya Serikali.
8. Malimbikizo ya madeni kutoka taasisi za Serikali yanairejesha nyuma Taasisi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inawapongeza watendaji wa vituo vya ZRA Kaskazini Unguja kwa kazi nzuri ya ufuatiliaji wanayoifanya na inashauri waendelee na juhudi hizo kwa ajili ya kuwavutia wateja na kupelekea makusanyo kuongezeka.
2. Kutokana na mazingira yasiyoridhisha kwa watendaji wa ZRA kituo cha Nungwi, Kamati inaitaka Wizara kuwajengea mazingira mazuri watendaji hao ili kuwajengea ari ya kazi.
3. Kwa ajili ya utendaji bora wa shughuli zake, Kamati inaishauri ZRA kuwa na mashirikiano ya moja kwa moja na halmashauri katika maeneo tofauti nchini.
4. Kamati inaishauri Wizara kufanya manunuzi ya dharura ya vifaa vya msingi kwa ajili ya utekelezaji bora wa kituo hicho.

## 2.7 MFUKO WA BARABARA ZANZIBAR (ZRF)

Mfuko wa barabara Zanzibar ni Taasisi ilioanzishwa kwa Sheria namba 2 ya 2001 inajulikanwa kama Zanzibar Roads Fund Act no 2 of 2001. ambayo ikafanyiwa marekebisho tena 2008. Majukumu makubwa ya mfuko huo wa Barabara ni kuhakikisha kuwa Fedha za matengenezo ya barabara zinakusanywa na vyombo vilivyowekwa na kuwasilishwa ZRF, kutoa fedha kwa matengenezo ya barabara kwa wakala mtekelezaji na kunawepo na matumizi mazuri ya fedha kwa usimamizi na ukaguzi wa ndani na nje.

Kwa kipindi cha Julai - Disemba 2022, Mfuko wa Barabara umeingiziwa jumla ya shilingi 4,418 bilioni. Kati ya hizo jumla ya shilingi 1.613 bilioni zimetumika. Ambapo shilingi 713.8 milioni zimetumika kwa kulipa madeni ya "retention" kwa barabara zilizokamilika ikiwemo Fuoni – Mambosasa – Mwera Wilayani na Gombani – Pagali Kwa mwaka wa fedha 2021-2022. Aidha, shilingi 322.8 Milioni zililipwa kwa kazi za matengenezo ya barabara zilizo chini ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ambazo

zinatekelezwa kupitia Wakala wa Barabara (Zanzibar Roads Agency) kwa ajili ya kulipa kazi za matengenezo ya barabara katika shughuli zifuatazo.

## CHANGAMOTO

1. Kuchelewa kukamilika kwa kazi mbalimbali zinazotokana changamoto ya mfumo mpya wa ununuzi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Nchi afisi ya Rais Fedha na Mipango kupitia Mfuko wa Barabara wakae Pamoja na Mamlaka ya Manunuzi ili kuweza kuyapatia ufumbuzi masuala yanayotokana mfumo mpya wa manunuzi.
2. Kamati inaitaka ZRF kuwapeleka wataalamu wake Kuwapeleka nje ya nchi Kwenda kusomea masomo ya uhandisi wa usafirishaji na Pamoja kuwafundisha uwezo wa kuvifanyia ukarabati (Services) vifaa na vipuri mbalimbali ili tupate kuondokana na utegemezi wa wataalamu wa kutoka nje ya nchi kila mara.
3. Iko haja ya Serikali kununua vifaa zaidi vya ujenzi wa barabara ili kutekeleza shughuli zinazopangwa kwa wakati.
4. Kamati inaiomba Serikali kuwalipa wananchi walioathirika na ujenzi wa barabara fidia zao kwa wakati ili kuendelea na shughuli nyengine za ujenzi wa Taifa.

## 2.8 OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI ZANZIBAR

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 inatekeleza majukumu yake ya matumizi kupitia fungu (F04) ambapo linajumuisha Programu Kuu mbili na Programu Ndogo nne (4). Programu kuu hizo ni Programu ya kuendeleza na kuratibu takwimu rasmi pamoja na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali.

Programu hizo zinajumuisha program ndogo ya ukusanyaji, uchambuzi na uwasilishaji wa takwimu rasmi za Kiuchumi na kijamii; Programu ya Uratibu wa shughuli za kitakwimu katika Mfumo wa Taifa wa Takwimu Zanzibar; Programu ya Utawala na Uendeshaji, Unguja pamoja na Uratibu na Programu ya Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Ofisi Ndogo Pemba.

### 2.8.1 MPANGO WA UENDELEZAJI TAKWIMU ZANZIBAR

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mpango wa Uendelezaji wa Takwimu Zanzibar (ZSDP) umekadiriwa kutumia jumla shilingi 13.22 bilioni kwa ajili ya uratibu na uendeshaji wa miradi katika kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo;

a) Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022;
b) Utafiti wa viashiria vya Ukimwi Tanzania HIV impact Survey (THIS);
c) Mpango kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania awamu ya pili, TSMP II;
d) Uchapishaji wa Ripoti ya Utafiti wa watu na wenye uwezo wa kufanya kazi 2020/21 (ILFS);
e) Utafiti wa Kufuatilia Kaya (National Panel Survey - NPS); na
f) Uimarishaji wa Takwimu za jinsia,

Katika kipindi cha Miezi sita Julai hadi Disemba 2022, mpango huu umepangiwa kutumia jumla ya shilingi 8.39 bilioni kwa ajili ya uratibu na uendeshaji wa mpango katika kutekeleza shughuli zifuatazo:

a) Sensa ya Watu na Makaazi ya mwaka 2022,
b) Utafiti wa viashiria vya Ukimwi Tanzania HIV impact Survey (THIS),
c) Mpango kabambe wa Uimarishaji Takwimu Tanzania awamu ya pili,
d) Uwasilishaji wa Ripoti ya Utafiti wa watu na wenye uwezo wakufanya kazi.
e) Utafiti wa Kufuatilia Kaya (National Panel Survey - NPS)
f) Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia.

## CHANGAMOTO

1. Ofisi inatumia fedha nyingi katika kufanya tafiti mbalimbali lakini matokeo ya tafiti hizo hubakia bila ya kutumika ipasavyo.
2. Kutokuwa na jengo la ofisi kwa upande wa Pemba.
3. Kupitwa na wakati kwa sera ya Idadi ya watu ya mwaka 2008.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kusimamia kikamilifu ujenzi wa ofisi ya Pemba na kuhakikisha shughuli hiyo inakamilika ifikapo mwaka 2024 kama ilivyopangwa.
2. Pamoja na tafiti mbalimbali zilizofanywa, Kamati inashauri utafiti maalumu wa hali ya mtoto wa Zanzibar juu ya hali ya udhalilishaji ifanywe ili tupate uelewa mpana wa tatizo lililopo nchini.
3. Ni wajibu wetu kutumia matokeo ya tafiti katika kupanga sera na sheria mbali mbali kwani tafiti hizo zimefanywa kwa gharama kubwa.
4. Kamati inashauri Sera ya Idadi ya watu ya mwaka 2008 ifanyiwe mapitio.
5. Kamati inashauri Taasisi za Serikali kutumia takwimu zinazotolewa na Ofisi ya Mtakwimu mkuu katika kupanga mipango yake kwani ndizo takwimu zinazokubalika nchini.

## 2.9 PROGRAMU YA URATIBU WA FEDHA ZA AHUENI YA UVIKO 19

Mwezi Oktoba 2021, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipatiwa dola za kimarekani 100 milioni sawa na shilingi 230 bilioni ikiwa ni sawa na 17.7% ya jumla ya mkopo wote wa 1.3 trilioni uliotolewa na IMF kwa Serikali ya Jamhuri ya Tanzania ili kuhuisha uchumi kutokana na athari ya UVIKO 19.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imezigawa fedha hizo kwa utaratibu maalum ambapo sekta ya elimu ilipatiwa jumla ya shilingi 68.6 bilioni, sekta ya afya ilipatiwa shilingi 80.1 bilion, Uchumi wa Buluu (Uwezeshaji wananchi) ilipatiwa jumla ya shilingi 33.8 bilioni, sekta ya nishati ilipatiwa jumla ya shilingi 11.4 bilioni, sekta ya maji ilipatiwa jumla ya shilingi 34.1 bilioni na jumla ya shilingi 1.9 bilioni zilitengwa kwa ajili ya Uratibu na Ufuatiliaji wa program hiyo kwa ujumla wake.

Kamati imebaini kuwa miradi ya UVIKO 19 iliyopo Zanzibar imechelewa sana kuanza kutokana na kuchelewa kwa mipango ya matumizi sahihi ya fedha za miradi hiyo. Hali hii imesababishwa na kukosekana kwa mipango ya muda mrefu ya nchi na hivyo kupelekea mara baada ya kupatikana fedha hizo miradi mbali mbali kuanza kubuniwa. Aidha, taratibu zetu za manunuzi zinazoongozwa na Sheria ya manunuzi na uondoaji wa mali za Umma Nam. 11 ya mwaka 2016 zinapelekea kudorora kwa shughuli zote zinazohitaji maamuzi ya haraka.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inawaomba vijana kuchangamkia fursa za mikopo zilizopo kwenye taasisi mbalimbali na kufanya matumizi sahihi ya mikopo hiyo ili kujikwamua katika dimbwi la umasikini.
2. Kutokana na umuhimu wa maji kwa maisha yetu, Kamati inasisitiza fedha zilizopangwa kuimarisha huduma za maji zitumike ipasavyo ili kuwaondolea usumbufu wananchi.
3. Kutokana na hali za vijana wetu waliothiriwa na matumizi ya dawa za kulevya, Kamati inashauri Serikali iwaendeleze katika shughuli zao walizojifunza mara baada ya kutoka kwenye sehemu za kurekebisha tabia, kwani kitendo cha kuwaacha mitaani kinaweza kuwapa fursa ya kurudia kwenye makundi maovu na kutofikiwa kwa lengo la Serikali.
4. Kamati inashauri fedha zinazotumika kwenye miradi hii ziendane na thamani halisi ya mradi.

## SEHEMU YA TATU

## AFISI YA RAIS, KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI

### 3. UTANGULIZI

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji ina jumla ya Idara 8, Ofisi Kuu Pemba na Taasisi 2 zinazojitegemea kama zifuatazo:-

### IDARA

1. Kamisheni ya Kazi
2. Ajira
3. Usalama na Afya Kazini
4. Uendelezaji na Uratibu wa Programu za Wananchi Kiuchumi
5. Maendeleo ya Vyama vya Ushirika
6. Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi
7. Uendeshaji na Utumishi
8. Mipango, Sera na Utafiti na
9. Ofisi Kuu Pemba

### TAASISI ZINAZOJITEGEMEA

1. Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA)
2. Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEF)

### 3.1 UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2022)

### FUNGU A07 (KAZI NA UWEZESHAJI)

Kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2022, ilitarajiwa kukusanya Mapato ya Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Moja na Moja, Laki Sita na Elfu Hamsini (Tsh. 1,101,650,000). Hadi kufikia Disemba, 2022, imefanikiwa kukusanya mapato ya Shilingi Milioni Mia Tisa Sitini na Nane, Laki Moja Sitini na Saba, Mia Sita na Hamsini (Tsh.968,167,650) sawa na asilimia 88 ya lengo

kutokana na Ada za Usajili na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika, Ada ya Ukaguzi wa Mikataba ya Ajira Nje ya Nchi na Ada ya Ukaguzi wa Maeneo ya Kazi na Vibali vya Kazi.

### 3.2 MATUMIZI JULAI HADI DISEMBA 2022

Wizara iliidhinishiwa matumizi ya jumla ya Shilingi Bilioni Nne, Milioni Mia Tatu Arobaini na Tano, Laki Moja na Elfu Nne, Mia Saba Sabini na Sita(Tsh.4,345,104,776). Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Sitini na Nane, Laki Sita Sitini na Tatu Elfu, Mia Tisa Arobaini na Saba(Tsh.1,768,663,947) ni kwa ajili ya Mishahara. Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Tano Sabini na Sita, Laki Nne Arobaini Elfu, Mia Nane Ishirini na Tisa(Tsh.2,576,440,829)Matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Kumi na Tisa na milioni mia tano (19,500,000,000) kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

### 3.3 FUNGU A08 (UCHUMI NA UWEKEZAJI)

Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Kipindi cha Julai – Disemba, 2022 kupitia fungu A08 (Uchumi na Uwekezaji lilikadiriwa kutumia jumla ya Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Mia Nne Sabini na Moja, Laki TatuSabini na Nane Elfu na Mia Mbili Tsh.2,471,378,200. Kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni Moja, Milioni Mia Saba Tisini na Tisa, Laki Moja Tisini na Nane Elfu, Mia Tisa na Tano Tsh 1,799,198,905 ni kwa ajili ya Mishahara; Shilingi Milioni Mia Sita Sabini na Mbili, Laki Moja Sabini na Tisa Elfu, Mia Mbili Tisini na Tano (672,179,295) kwa ajili ya Matumizi mengineyo na Shilingi Bilioni Kumi na Tano na Milioni Mia Moja (15,100,000,000) ni kwa Miradi ya Maendeleo.

### 3.4 PROGRAMU YA FEDHA ZA IMF (COVID FUNDS)

Programu ya Fedha za kupunguza athari za UVIKO 19 kwa wajasiriamali ilizinduliwa rasmi tarehe 12 Februari, 2022 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dk. Hussein Mwinyi, katika Ukumbi wa Mhe. Idrissa Abdulwakil, Kikwajuni.

Utekelezaji wa mradi huu unasimamiwa na Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (ZEEA) ambapo Taasisi hii ina maeneo makuu mamne (4) ya utoaji wa huduma kwa Jamii ambayo ni:

i. Mafunzo.
ii. Mikopo/Mitaji,
iii. Masoko.

iv. Miundombinu wezeshi.

Programu hii ina aina mbili za mikopo kwa Wajasiriamali na Wafanyabiashara wadogo wadogo, wadogo na wakati ambazo ni:

a) Mikopo ya vikundi.

b) Mikopo ya Mtu mmoja mmoja( Wawekezaji wazawa -Local Investors).

Aina zote hizi za mikopo zina taratibu zake zilizopangwa kwa pamoja kati ya Wadau wa Programu hii ambao ni Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji na Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kwa upande mmoja, na Benki ya CRDB, kwa upande mwingine. Muongozo huo unaitwa "Business Model for Inuka Loans". Kwa ujumla unasema kuwa, kwa mikopo ya vikundi, kiasi cha juu cha mikopo kwa mkopo mmoja wa kikundi ni shilingi 100,000,000 milioni na kama wajasiriamali wataamua kuchukua mkopo wa mtu mmoja mmoja ndani ya kikundi (Solidarity Loans) kima cha juu cha mkopo hakitazidi shilingi 15,000,000 milioni kwa mjasiriamali mmoja ndani ya kikundi. Kwa upande wa mikopo ya Local Investors, kima cha juu kabisa kwa mujibu wa Muongozo ni shilingi 300,000,000 milioni. Aidha, mikopo yote hiyo inatakiwa irejeshwe ndani ya kipindi cha miaka miwili.

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2022 jumla ya mikopo 2,625 yenye thamani ya shilingi 16,828,133,520.17 imeshatolewa Unguja na Pemba. Mikopo hiyo imewanufaisha Wajasiriamali na Wafanyabiashara ambao wanajishughulisha na shughuli mbalimbali zikiwemo, Bodaboda, Kilimo, Ufugaji wa nyuki, Uchongaji wa mbao, uchomaji wa vyuma, uuzaji wa vyakula na kazi za mikono.

Jumla ya mikopo 1,121 yenye thamani ya shilingi 10,183,472,280 bilioni imetolewa kisiwani Unguja ambayo imetolewa kwa wajasirimali 8,145 (2,705 Wanaumena 5,448 Wanawake). Kwa upande wa Pemba, jumla ya mikopo 1,504 yenye thamani ya shilingi 6,644,661,240.17 imetolewa ambayo kwa wajasiriamali 8,755 (3,174 Wanaume na 5,581 Wanawake). Kwa ujumla, Mikopo yote hiyo imewanufaisha wananchi 16,908.

## CHANGAMOTO

1. Marejesho madogo ya mikopo kutokana na dhana ya kwamba ni fedha za Serikali na wananchi hawalazimiki kulipa.
2. Mara baada ya kupatiwa mafunzo, wajasiriamali walio wengi hushindwa kupata fedha za ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kufanyia kazi jambo ambalo linapelekea kudumaa kwa fani zao.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kutokana na hali duni za kiuchumi za wananchi wengi, ni jambo la busara sana kwa Wizara kuwashika mkono wajasiriamali hawa mara baada ya kuwapatia mafunzo ili kuwapatia vitendea kazi na kuzalisha kwa kutumia ujuzi waliopatiwa.
2. Ni wajibu wa Serikali Kupitia wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kuwaongoza wajasiriamali juu ya shughuli za kufanya kabla ya kupatiwa mikopo yao ili kuitumia mikopo hiyo kwa njia sahihi.
3. Mapitio ya mara kwa mara yanapaswa kufanywa na Wizara ili kuhakikisha wajasiriamali wetu wanaenda kwenye mwelekeo sahihi. Wazalishaji wa asali wanapaswa kutizamwa zaidi ili kuhakikisha uzalishaji wao unaongezeka kwa ajili ya kufanya marejesho ya mkopo kwa wakati uliopangwa.
4. Kamati inaunga mkono suala la uanzishaji wa mfumo wa mikopo ambao utawatambua wakopaji wote na kuwapatia huduma kwa mujibu wa muda wa kuwasilisha maombi yao (first in first served).
5. Kamati inashauri Serikali kusimamia vyema fedha za mikopo ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili zirejeshwe kwa wakati na kuwanufaisha wajasiriamali wengine. Katika kufikia lengo hili, Kamati inawaomba Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa kuvisimamia vikundi vya wajasiriamali waliomo kwenye maeneo yao na kuhakikisha wanafanya shughuli zitakazowawezesha kufanya marejesho ya mikopo yao.
6. Kamati inashauri maeneo yaliyetengwa kwa ajili ya viwanda vya kusarifu asali kuwekewa uzio na kupandwa miti ili yaweze kuwekewa mizinga ya nyuki na kufanya shamba darasa kwenye maeneo hayo.

## 3.5 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI VITEGA UCHUMI ZANZIBAR (ZIPA)

Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar ni Taasisi ya Serikali inayofanyakazi chini ya Sheria ya Mamlaka ya kukuza na kulinda Uwekezaji Zanzibar Na. 14, 2018. Jukumu la msingi la Mamlaka hii ni kutekeleza sera na Sheria ya Uwekezaji kikamilifu kwa nia ya kuwavutia wawekezaji wenye tija kwa manufaa ya nchi na wananchi wake.

Serikali, kupitia Mamlaka hii imeelekeza nguvu zake katika kutangaza na kusimamia Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2008 katika sekta zote zinazohusika. Aidha, mkazo maalum umewekwa

kwenye uimarishaji wa uchumi wa buluu ikizingatiwa kuwa jiografia ya Zanzibar ni visiwa na ina uwanja mpana wa kuimarisha sekta hiyo.

## CHANGAMOTO

1. ZIPA imekuwa ikikumbana nachangamoto ya upimwaji wa ardhi,jambo ambalo linazorotesha jitihada za uwekezaji nchini,kwani mfumo mzima wa upimaji wa ardhi umekua ukichukua muda mrefu.
2. Dhana ya one stop center Kwa upande wa kisiwani Pemba bado haijasimama sawa sawa kutokana na kukosekana Ofisi kwa baadhi ya Taasisi zinahusika na utaratibu wa uwekezaji, jambo ambalo linapelekea mlolongo mkubwa kwenye kupata vibali vya uwekezaji.
3. Uhaba wa usafiri kwa ajili ya kukagua maeneo ya Uwekezaji kisiwani Pemba.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Ni vyema Serikali kuijengea Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar Jengo ambalo litaendana na hadhi ya Taasisi hiyo na kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini.
2. Ili tuyafikie malengo ya Serikali yetu ya awamu ya nane ya kuwainua wananchi kiuchumi kupitia uwekezaji, Kamati inashauri Taasisi za Serikali kuwa na nia ya dhati katika utendaji wao na kuacha tabia ya kutupiana majukumu baina ya Taasisi moja na nyengine.
3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara husika kuwapa mamlaka maafisa wanaohusiana na kituo cha 'One Stop Centre' kufanya maamuzi yote yanayohusiana na shughuli mbali mbali za Taasisi zao.
4. Kamati inaishauri Wizara kupitia ZIPA kuwa makini Zaidi kwenye zoezi la utoaji wa vibali kwani wapo watu wanaokuja hapa nchini kwa sura ya uwekezaji lakini kiuhalisia ni wadanganyifu ambapo huja na dhana nzima za miradi na kupewa maeneo na baadae huondoka nchini bila ya taarifa.
5. Kamati inashauri Wizara kupitia ZIPA kazi zote ambazo hazihitaji utaalamu na zinawezekanwa kufanya na wazawa basi wapewe wazawa, na hizo za utaalamu wapelekwe wazawa wakajifunze jambo hilo litaondosha tatizo la ajira kwa vijana.
6. Kamati inashauri tena Wizara kupitia ZIPA kuhakikisha kuwa mwekezaji yeyote anaehitaji kuekeza nchini, hususan katika maeneo ya vijijini, anasimamiwa ipasavyo ili ajira za miradi hiyo zinawahusisha wanakijiji walioko karibu na miradi hiyo zirudi kwa wanakijiji hao.

7. Kamati inaishauri Wizara kupitia ZIPA, kufanya mazungumzo na ZAWA kwenye maeneo yote ya uwekezaji kwamba kabla ya kuanza kwa miradi hiyo ZAWA wawe washaweka miundombinu ya maji ili kuiepushia hasara Serikali kwa kuvunja na kujenga upya miundombinu ya barabara na maji kila mara.
8. Kamati inaishauri Serikali kupitia ZIPA kufanya uajiri mpya Kwa vijana kwani watendaji wengi wa mamlaka hiyo umri wao wa kustaafu umekaribia hivyo wanapaswa kuajiri vijana wapya ili wapate kujifunza kutoka kwa watumishi wenye uzoefu.
9. Kamati inaitaka Serikali kupitia ZIPA kuyawekea uzio maeneo yote huru ya Uwekezaji kwani yamekua yakivamiwa Sana na wananchi kwa shughuli mbalimbali.
10. Kamati inasikitishwa na kukosekana ufuatiliaji kwenye kulitafutia hati miliki shamba la makurunge liliopo wilaya ya Bagamoyo, Mkoa wa Pwani, Tanzania Bara kwani eneo hilo linazidi kuvamiwa na wananchi, hivyo Kamati inaitaka Wizara kulitafutia ufumbuzi wa haraka jambo hilo.

## 3.6 HOTELI YA FUNDU LAGOON

Hoteli hii inapatikana wilaya ya Mkoani, Mkoa wa kusini Pemba na ilianzishwa mwaka 2000 na Wawekezaji raia wa Uengereza. Shughuli zinazofanywa kwenye hotel hii ni kutoa huduma zote za hotel zikiwepo huduma za malazi na migahawa pamoja na michezo mbalimbali ya bahari (Diving). Sambamba na hilo, Hotel hii imejikita kwenye kutunza mazingira ya uoto wa asili wa maeneo yake yote.Changamoto ya usafiri inaifanya Hoteli hiyo kutoa huduma ya usafiri kwa wanakijiji mara 2 kwa siku kwa kutumia boti zake.

### CHANGAMOTO

1. Kuna tatizo kubwa la ukosefu wa umeme kwenye eneo linazonguka hotel na kijiji chote.
2. Hoteli hiyo na kijiji kinachozunguka eneo linakumbana na ukosefu mkubwa wa maji.
3. Kutoka barabara kuu ya kuelekea eneo lilipo hoteli haiku katika hali inayoridhisha na ikiwa ni kipindi cha mvua njia hiyo haifikiki kabisa. Njia pekee ya kufika eneo hilo ni kutumia boti.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaiomba Wizara kupitia ZIPA kumwita mwekezaji wa Hoteli ya Fundu Lagoon kumzawadia cheti kutokana kulinda kwake mazingira asilia.
2. Kamati inaiomba Wizara ikae na Wizara ya Afya ili ifanye utaratibu wa kupeleka kituo cha afya kwenye kijiji hicho kwani wananchi wanateseka sana na ili kufika hospital ni lazima watumie boti za hoteli hiyo kwani njia ya barabara sio rafiki kwa wananchi hususan kwa mama wajawazito.
3. Kamati inaishauri Wizara kumshauri Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenda kulitembelea eneo la hoteli hiyo kwani ni kivutio kizuri cha Utalii wa kimazingira na mheshimiwa Rais pindi atakapofika eneo hilo kamati inamini kijiji hicho kitafunguka zaid kiutalii.
4. Kamati inaiomba Wizara kumtumia mwekezaji wa Hoteli hiyo kama mfano kwa wawekezaji wengine kuwafundisha jinsi ya kufanya uwekezaji bila ya kuathiri mazingira asilia ya maeneo wanayotaka kuwekeza.
5. Kamati inaiomba Wizara kukaa na Wizara zinazohusika na sekta za umeme, maji na Barabara ili kuweza kufika kwenye eneo hilo na kuwaondolea changamoto wananchi wanaozunguka eneo hilo.

## 3.7 KIWANDA CHA MAJI CHA WATERCOM

Kiwanda cha maji cha Watercom kipo Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba ni sehemu ya tawi la kiwanda kikuu kilichopo Mkoa wa Dar es salam. Kiwanda hiki kilianza kujengwa Januari 2021 na ilipofika November 2022 kiwanda kilianza kuendesha shughuli zake kwa njia ya majaribio. Uwekezaji wa kiwanda hiki umegharimu dola za kimarekani laki 4.63 na kina uwezo wa kuzalisha lita za maji milioni 58 kwa siku, kiwanda hiki kilichukua uamuzi wa kufika kisiwani pemba baada kuitikia wito kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wa kukifungua kisiwa cha Pemba kiuchumi na Zanzibar kwa ujumla. Sambamba na huduma za uzalishaji wa maji, kiwanda hicho pia kinatoa huduma za kuwapa wananchi maji bure kwa kutoa mipira ya maji hadi kwenye vijiji vinavyozunguka kiwanda hicho.

## CHANGAMOTO

1. Kiwanda kinakabiliwa na tatizo kubwa la ukosefu wa umeme mkubwa unaohitajika kwa ajili ya uzalishaji. Pia, umeme unaotumika kiwandani hapo hauko stable na unazimwa mara kwa mara jambo ambalo linazorotesha uzalishaji wa maji na kumtia hasar mwekezaji.
2. Ubovu wa barabara inayoelekea kiwandani hapo unaopelekea usumbufu kwa wateja.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaigiza Wizara kupitia Afisi kuu pemba kuhakikisha wafanyakazi wa kiwanda cha Watercome wanapatiwa mikataba ya kazi na pia kusajiliwa kwenye mfuko wa hifadhi ya jamii (ZSSF).
2. Kamati inaitaka Wizara kupitia ZIPA pindi kiwanda hicho kitakapofikia hatua ya kutengeneza vinywaji baridi kama vile juisi basi mamlaka inapaswa kukilazimisha kiwanda hicho kutumia malighafi za matunda zinazopatikana kwenye kisiwa cha Pemba.

## 3.8 KAMISHENI YA KAZI

Kamisheni ya Kazi ipo chini ya Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na imeanzishwa chini ya Sheria ya Ajira Namba 11 ya mwaka 2005. Jukumu hasa la Kamisheni ya Kazi ni kusimamia utekelezaji wa Sheria za Kazi katika utumishi wa umma na sekta binafsi kwa hapa Zanzibar. Kamisheni ya Kazi ina jukumu la kufanya ukaguzi kazi kwa Taasisi zote za sekta binafsi na kusimamia Ajira za wafanyakazi wa kigeni, kuthibitisha mikataba ya wafanyakazi wazalendo na wageni na kusimamia uimara wa mahusiano mema kati ya waajiri na waajiriwa katika sehemu ya kazi.

## CHANGAMOTO

1. Baadhi ya Taasisi binafsi nchini huajiri maafisa utumishi ambao sio wanzanzibari jambo ambalo linapelekea maafisa utumishi hao kuajiri watu wa maeneo yao na kuwaacha Wazawa hata kama wana sifa zinazohitajika.

2. Upungufu wa watendaji katika nafasi mbalimbali za kiutumishi ambapo Kamisheni imepungukiwa na wakurugenzi wawili (2) wakati Kamati ilipoitembelea jambo ambalo linapelekea kuzorota kwa baadhi ya kazi.
3. Upungufu mkubwa wa maafisa kazi (wakaguzi) wa kupitia na kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali jambo linazorotesha utendaji kazi wa kamisheni hiyo.
4. Utaratibu wa sasa wa kuwasilisha fedha zote zinazokusanywa kutokana na shughuli mbalimbali za Kamisheni hazina bila ya kubakisha chochote kwa ajili ya matumizi ya Taasisi yenyewe huleta changamoto pale Kamisheni inapohitaji kufanya matumizi.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Kamisheni ya kazi kusimamia Taasisi binafsi ili kuhakikisha kuwa nafasi zote za maafisa utumishi hapa nchini wapewe wazanzibari na Kamisheni inapaswa kutoa taarifa (notice) hiyo kwa Taasisi binafsi hususan kwenye sekta ya hoteli.
2. Kamati inaishauri kamisheni ya kazi kuzijaza nafasi hizo mbili ili kuweza kuleta ufanisi Zaidi wa shughuli za kamisheni hiyo.
3. Kamati inaitaka Kamisheni ya kazi kufuatilia usalama wa wafanyakazi waliopo nje ya nchi kwa kufanya ziara kwenda kuwakagua hukohuko badala ya kusubiri taarifa za kibalozi tu.
4. Kamati inaigaiza Kamisheni ya kazi kuwafuatilia na kuwachunguza mawakala, ili kujiridhisha kuwa kazi walizozitangaza na wanazokwenda kupewa vijana wetu ni zile walizoziomba kwani kumekua na utitiri wa biashara chafu zinazofanyika huko na vijana wetu wamekua wahanga wa biashara hizo zisizohalali.
5. Kamati inaitaka Serikali iwachie Kamisheni ya Kazi japo kiwango Fulani cha fedha wanachokikusanya ili waweze kujiendesha mambo yao wenye kwani kwa kusubiria pesa za matumizi mengineyo(OC) Kamisheni Kamisheni itashindwa kutimiza malengo yake.
6. Kamati inaitaka Kamisheni ya kazi kuendelea kufanya operation za mara kwa mara ili kuweza kubaini Taasisi zilizokataa kulipa kima cha chini cha mshahara uliowekwa na Serikali.

## 3.9 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Wakalawa wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ni Taasisi ilioanzishwa na Sheria namba mbili (2) ya mwaka 2022. Madhumuni ya kuanzisha Wakala huu ni kusimamia masuala yanayohusiana na

uwezeshaji kiuchumi kwa wajasiriamali na wafanya biashara ndani ya Zanzibar ili kuwakuza na kuanzisha fursa za ajira. Aidha, Wakala huu utakua na majukumu ya kutoa huduma zote za mikopo,mafunzo, miundo mbinu na masoko kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wote kwa lengo la kushajiisha maendeleo endelevu na kuendeleza Miradi yao ya Kiuchumi itakayowapatia kipato cha kujikimu kwa maisha yao ya kila siku na familia zao.

Ili kufikia malengo hayo kwa wepesi, Wakala inaendeleza vituo viwii vya kulea wajasiriamali (incubation center) vilivyopo Mbweni na Kinyasini. Vituo hivyo vinatoa mafunzo ya uzalishaji wa vyakula na vinywaji, biashara na ujasiriamali pamoja na elimu ya msingi ya ICT. Wanafunzi wa vituo hivyo wanatoka katika wilaya zote za visiwa vya Zanzibar na hupatiwa mafunzo vituoni humo kwa muda wa mwaka mmoja na baada ya kuhitimu wana wajibu wa kuendeleza shughuli za uzalishaji na kuwafunza wengine elimu waliyoipata.

Kwa upande wa kituo cha Mbweni, jumla ya mashine 32 za kuzalisha bidhaa mbali mbali zinapatikana kituoni hapo ambapo wanafunzi wanalelewa na kufunzwa namna ya kuzitumia mashine hizo katika kuzalisha bidhaa bora.

## CHANGAMOTO

1. Wakala bado hauna muundo wa utumishi.
2. Wakala hauna jengo la ofisi hadi sasa.
3. Kutokuwa na nembo ya utambulisho wa Wakala.
4. Wakala hauna gari kwa ajili ya ufuatiliaji wa shughuli zake.
5. Uhaba wa malighafi za kuzalishia bidhaa za maziwa nchini kutokana na ukweli kwamba wafugaji wetu wanafuga kwa kiwango kidogo (subsistence).
6. Baadhi ya wajasiriamali hushindwa kuzalisha wakiwa nje ya usimamizi na hurudi chuoni kwa ajili ya kupata mwendelezo wa shughuli zao.
7. Ufinyu wa bajeti unaopelekea ufinyu wa huduma za kituo cha Mbweni.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kupitia Wakala wa Uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kufungua ofisi zao kwa kila Wilaya ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wajasiriamali.
2. Kamati unautaka Wakala kupitia program ya INUKA wasiishie kwenye Wilaya nne tu za Pemba bali program hiyo inapaswa kuendelea kwa wilaya nyengine zilizobakia kwa upande wa Unguja.

3. Kamati inaushauri Wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoa mikopo kwa njia ya electroniki ili kufanya shughuli hiyo kwa urahisi na kuhifadhi kumbukumbu za mikopo kwa muda mrefu.
4. Kamati inaishauri Wizara kutoziingiza fedha zote za ahueni ya UVIKO 19 kwa benki moja pekee bali fedha hizo zigawanye kwenye benki nyengine na zisiwekwe kwenye benki moja kama ilivyosasa ili kuleta ushindani wa kibiashara utakaopelekea kuongezeka kwa ufanisi wa kazi.
5. Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Uwezeshaji kuwatafutia masoko wajasiriamali wadogo kwani bila ya soko la uhakika lengo la kuwainua wajasiriamali halitafanikiwa.
6. Kutokana na mwamko mkubwa wa wazalishaji wa viwanda vidogo vidogo nchini, wakati umefika kwa Serikali kuwawezesha wazalishaji wa malighafi za kuendeshea biashara kama wafugaji wa maziwa kuwa na ufugaji mkubwa na wa kisasa ili kukidhi mahitaji ya wazalishaji wa bidhaa za maziwa nchini.
7. Wizara iwaendeleze zaidi walezi wa vituo hivi ili kuwafanya wawe wajuzi wa mabo makubwa zaidi na kuacha utegemezi wa wataalamu kutoka nje ya nchi.
8. Uzalishaji wa bidhaa mbali mbali katika vituo vyetu hivi unahitaji kutangazwa ili kuwapasha habari wanunuzi juu ya bidhaa zetu.
9. Kamati inashauri Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji kushirikiana na Wizara inayohusika na biashara katika kutafuta muarobaini wa ukosefu wa vifungashio vya bidhaa mbali mbali vinavyokwenda na wakati.
10. Ili kuzalisha wajasiriamali wazuri, Kamati inapendekeza somo la ujasiriamali lipewe kipaumbele kwenye mitaala ya vyuo vyetu.
11. Wakala uwe na kawaida ya kujitangaza kupitia vyombo vya habari ili wananchi waelewe juu ya shughuli wanazoziendesha.
12. Kamati inaitaka Wizara kusimamia wawekezaji ili kuwapatia wafanyakazi wa viwandani vifaa na elimu ya kujikinga na majanga katika kazi. Aidha, uangalizi wa mara kwa mara wa afya zao unahitajika ili kubaini haraka changamoto za kiafya zinapojitokeza.

### 3.9.1 VIKUNDI VYA USHIRIKA

Dhamira kuu ya Serikali ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi ni kupunguza wimbi la umasikini kwa kuwawezesha wananchi kwa njia mbalimbali ikiwepo kwa njia za mikopo nafuu ambapo wananchi hukopeshwa kiasi cha fedha na baadae kurejesha fedha hizo kidogokidogo kupitia shughuli za kiuchumi walizozianzisha. Kabla ya Serikali

kuamua kutunga sheria ya kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Vikundi vyote na jumuia mbalimbali zilizoundwa kwa lengo la kujikwamua kiuchumi zilikua chini ya Taasisi iliokua ikijulikanwa kama Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Mfuko huo ulikua na lengo kuu la kuimarisha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa Wananchi. Kwa kipindi cha 2022/2023 Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi katika mizunguko yake minne (4) ya kazi ilifanikiwa kuvitembelea vikundi mbalimbali kama ifuatavyo;

a) Amkeni cooperative,
b) Kituo cha asali pujini,
c) Atoe ni karima,
d) Tumshukuru mungu,
e) Nia safi dunga kiembeni,
f) Kituo cha asali kizimbani na
g) Shukrani zetu bambi.

## CHANGAMOTO

1. Vikundi vingi vya wajasiriamali havijui fursa za mikopo zilizopo nchini na hushindwa kujiendeleza zaidi katika shughuli zao za kiuchumi. Kamati ilishuhudia kikundi cha wafuga samaki cha Amkeni kilichopo Kojani kisiwani Pemba wanachama wake hawana taarifa yoyote juu ya fursa hizo ingawa walikuwa ni wahitaji wa huduma hiyo.
2. Uhaba wa vitendea kazi katika vikundi vya wajasiriamali ni jambo linapelekea kuzorota Kwa kazi zao.
3. Wizi ni changamoto kubwa inayowakumba wanavikundi hususan wanaojishughulisha na ufugaji wa mazao ya baharini ambapo Kamati ilielezwa kadhia iliowakuta wanakikundi cha Amkeni Kojani ambapo siku chache kabla ya kuvuna samaki waliowafuga, samaki wote waliibiwa.
4. Maeneo mengi yanayomilikiwa na wanavikundi bado hayajasajiliwa na wanavikundi hao hawana umiliki wa ardhi hizo.
5. Vikundi vingi maeneo wanayoendesha shughuli zao hua wanakodi na kwa kuwa upatikanaji wa faida kutokana kazi zao hua ni mdogo inapelekea hata ulipaji wa kodi wa maeneo hayo kutoridhisha.

6. Vikundi vingi vinakufa kutokana watendaji wa vikundi hivyo kuwa na shughuli mbalimbali hivyo miradi yao kubaki haina mshughulikiaji.
7. Vikundi vingi vinashindwa kufikia malengo yao kutokana na kuchukua mikopo na kushindwa kujua ni aina gani ya miradi wanapaswa kufanya.
8. Uchelewaji wa fedha za mikopo kwa vikundi vya wajasiriamali mbalimbali nchini ni jambo linalowarejesha nyuma wajasiriamali hao kwani thamani za bidhaaa walizoombea mikopo hiyo hupitwa na wakati na bidhaa hizo hua zishapanda bei.
9. Vikundi vingi vinakua havina maendeleo kutokana na ukweli kwamba wengi wa wanavikundi hivyo ni jinsia ya kike hivyo wanapoolewa na kupata ujauzito ufanisi wa vikundi hivyo husuasua.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Serikali kupitia Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi kuendelea kutoa elimu ya mikopo kwa vikundi mbalimbali kwani bado wanavikundi wengi hawana elimu hizo.
2. Kamati inaitaka Serikali kupitia Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi kuwaalika waheshimiwa Wawakilishi kwani wao ndio waliokaribu na jamii hizo, na hata inapotekea ugumu wa kurejesha mikopo hiyo wao ndo itakua kiunganishi baina wanakikundi na Wakala.
3. Kamati inashauri Wakala pindi wanapotoa mikopo kwa vikundi kuwafuatilia kila hatua na wasisubiri tu hadi tarehe ya marejesho ifike. Kufanya hivyo kutawafanya wanavikundi kujua kuwa wanafuatiliwa na watafanya kazi kwa bidii ili kurejesha mikopo hiyo na kutimiza malengo yao.
4. Kamati inaitaka Wizara kupitia wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi kuwatangaza vijana waliofanikiwa kutokana na mikopo na miradi mbalimbali ya uwezeshaji ili iwe chachu kwa vijana wengine kwa kutumia vyombo vya habari au kwa kutumia mitandao mbalimbali ya kijamii.
5. Kamati inaitaka Wizara kuwatumia maafisa wake wa habari kuzitangaza kazi za uwezeshaji wananchi kwani jambo hili litasaidia kuinua soko la biashara kutokana na kazi zao kuonekanwa katika maeno tofauti ndani na nje ya nchi.

6. Kamati inaitaka Wizara kupitia Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi kama ndio mlezi mkuu wa wajasiriamali wote hapa nchini kuwatafutia masoko ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi.
7. Kamati inaishauri Wizara kupitia Wakala wa Uwezeshaji wananchi Kiuchumi kuwapa elimu wakulima kulima mazaodawa kwani yamekua na soko kubwa kwenye soko la dunia.

### 3.9.2 MAENEO HURU YA UWEKEZAJI - MICHEWENI.

Serikali ya awamu ya nane (8) inayoongozwa na Dkt Hussein Ali Mwinyi, imedhamiria kukifungua kisiwa cha Pemba kiuchumi ambapo uendelezwaji wa maeneo huru ya Uwekezaji lililopo wilaya ya Micheweni limekuwa ni kipaumbele maalum. Katika utekelezaji wa azma hiyo ni lazima kuwepo kwa barabara zilizobora na nzuri.

Eneo lote la maeneo huru ya Uwekezaji lililopo wilaya ya Micheweni lina ukubwa Hekta 808.4, eneo hili limegawanya katika sehemu A na B. Katika kutimiza wajibu wake, Serikali kupitia Afisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji inaendelea na harakati za ujenzi wa miundombinu kwenye eneo hilo ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje.

Hadi sasa miundombimu ya umeme imeshafika katika eneo hilo na ujenzi wa barabara wa kiwango cha lami unaendelea ambapo barabara yenye urefu wa kilomita zaidi ya 13 inajengwa. Hadi utakapomalizika mradi huo unategemewa kugharimu jumla ya shilingi 6.9 bilioni.

### CHANGAMOTO

1. Kasi ndogo ya ujenzi kutokana na zoezi la upatikanaji wa vifaa kuchukua muda mrefu kwa mujibu wa taratibu za manunuzi.
2. Upungufu wa watendaji kwa Wakala wa barabara Zanzibar jambo linalopelekea kukosekana umakini kwenye usimamiaji kazi. Watendaji hao hushindwa kujigawa kutokana na wingi wa kazi zao.
3. Mafuta ya kuendeshea mashine nzito za vifaa vya ujenzi yanapatikana mbali hali inayozorotesha zoezi la ujenzi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuharakisha suala la ulipaji wa fidia kwa wananchi walioathirika na shughuli za eneo la uwekezaji.
2. Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji inapaswa kuchukua hatua za haraka kila inapokutana na changamoto inayotaokana na mamlaka nyengine ili kuondoa matatizo hayo.
3. Kamati inaitaka Wizara kushirikiana na Mamlaka ya Maji ZAWA katika hatua iliyopo ya ujenzi wa barabara ili kuweka miundo mbinu ya maji kabla ya kukamilika ujenzi wa barabara ili kuepusha uharibifu barabara hizo baada ya ujenzi kumaliza kama unavyojieleza kwa maeneo mengine.
4. Kamati inaagiza ujenzi umalizwe kwa haraka sana kwani kadri ujenzi unavyochelewa na gharama ya vifaa vya ujenzi navyo vinapanda na kupelekea kuitwisha mzigo Serikali
5. Kamati inaitaka Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kutenga maeneo mengine kwa ajili ya wanachi waliokubali kutoa ardhi zao kwa ajili ya uwekezaji ili waweze kuendesha shughuli zao za kiuchumi na kuendesha maisha yao.

### 3.9.3 KITUO CHA KUSARIFU MAZAO YA ASALI PUJINI

Kituo cha kusarifu asali kilichopo Pujini ni miongoni mwa vituo vilivyojengwa kwa fedha za Uviko 19, kituo hiki kinatumika kutoa mafunzo ya wafugaji wa nyuki na usarifu wa asali, ambapo mafunzo hayo hutolewa kwa siku 14, kituo hicho kina madarasa makubwa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 kwa wakati mmoja, ambapo wanapomaliza mafunzo hayo wanapaswa kukopeshwa vifaa vyote vinavyohusika na mambo ya uvunaji wa nyuki, ambapo seti nzima ya vifaa vyote kwa gharama ya shilingi laki 130,000 ambapo kila mkulima atapewa mizinga 5 kwa gharama ya shilingi za kitanzania 380,000 na marejesho yake yatakua kwa miaka 2. Hadi kufikia sasa wanafunzi waliopata mafunzo ya ufugaji na usarifu wa nyuki ni 350, Serikali mpaka sasa imeshandaa mizinga 1800 ambapo watapewa wanavikundi tofauti ambao wamepata mafunzo hayo.

## CHANGAMOTO

1. Wafugaji wengi waliopatiwa mafunzo hawana uelewa ya kwamba vifaa wanavyopewa ni vya mikopo na wanapaswa waurejeshe mkopo huo.
2. Changamoto ya wadudu wa waharibifu wanaoharibu asali.
3. Zanzibar hakuna sera ya ufugaji nyuki hadi sasa.
4. Wizi wa mizinga ya nyuki umeshamiri.
5. Vikundi vimekua na watu wengi, mizinga 4 hadi 5 wanayopewa wanavikundi haviwatoshelezi.
6. Kumekuwepo na changamoto ya utengenezaji asali feki lakini zikiwa na majina (brand) ya kutoka Pemba.
7. Ukosefu wa usafiri haswa gari kwenye kufualititilia shughuli nzima za usarifu wa asali.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka wizara kuharakisha suala la ugawaji wa mizinga ya nyuki kwani ufugaji wa nyuki unahitaji jua na karibu wanavyochelewa kipindi cha mvua cha masika kinakaribia na pindi masika yatakapofika yataharibu uzalishaji wa asali.
2. Kamati inaitaka wizara iwape elimu ya bima kwa wanavikundi kwani kazi yao ufugaji nyuki ina hitaji tahadhari kubwa.
3. Wizara iandae utaratibu wa watu binafsi wasiokuwa wanavikundi kuwapa fursa ya kununua mizinga kwa njia ya pesa taslim ili nao mtu mmoja mmoja aweze kupata fursa za ufugaji.
4. Kamati inaitaka Wizara kutengeneza mazingira ya uwekaji wa mizinga katika maeneo hayohayo ya kituo ili wanafunzi wapate kufanya mafunzo ya nadharia na vitendo hapo hapo.

## SEHEMU YA NNE

### WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

### 4. UTANGULIZI

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeundwa na Idara sita na taasisi nne zinazojitegemea kama ifuatavyo:

IDARA

i. Uendeshaji na Utumishi
ii. Mipango, Sera na Utafiti
iii. Uratibu wa Uchumi wa Buluu (Ukijumuisha Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi)
iv. Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini
v. Hifadhi za Baharini
vi. Afisi ya Afisa Mdhamini – Pemba

TAASISI

i. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Bahari;
ii. Kampuni ya Uvuvi;
iii. Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Company);
iv. Mamlaka ya Kudhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta (Zanzibar Petroleum Development Authority)

### 4.1 UKUSANYAJI MAPATO KWA KIPINDI CHA MIEZI SITA (JULAI- DISEMBA 2022)

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya shilingi 2,259,412,274 bilioni kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2022, Wizara ilikadiriwa kukusanya shilingi 1,180,145,380 bilioni na imekusanya jumla ya shilingi 1,753,570,513.2 bilioni sawa na asilimia 148.59 ya makadirio

### 4.2 MATUMIZI JULAI HADI DISEMBA 2022

Kwa upande wa matumizi, Wizara imeombewa Jumla ya shilingi 89,662,400,000 bilioni. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,429,800,000 bilioni kwa ajili ya Mishahara; shilingi 3,269,000,000 bilioni ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi 2,407,800,000.00 bilioni ni RUZUKU kutoka SMZ (shilingi 320,000,000.00 ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini

(ZAFIRI), shilingi 1,775,300,000.00 bilioni ni kwa ZPRA na shilingi 312,500,000.00 milioni ni kwa ZAFICO). Kwa kutekeleza programu na Miradi ya Maendeleo Wizara imeombewa jumla ya shilingi 81,555,000,000 bilioni.

Aidha, katika kipindi hicho Wizara imepatiwa TZS 19,744,671,151 ambapo kati ya fedha hizo TZS 2,922,728,675 ni matumizi ya kawaida na TZS 16,821,942,476 kwa kazi za Maendeleo.

Matumizi halisi ya fedha hizo TZS 2,922,728,675 ambapo TZS 1,846,413,570 ni kwa matumizi ya kawaida, TZS 1,445,230,570 mishahara; TZS 401,183,000 Matumizi Mengineo na **TZS** 1,076,315,105 ni za Ruzuku kwa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI), Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO).

Kwa kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Disemba, 2022 Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC) imeingiziwa Jumla ya TZS 1,560,685,462.50. Kampuni katika kipindi hiki imefanya matumizi ya jumla ya TZS 885,999,897.00 kati ya fedha hizo TZS 729,002,009.00 zilitumika kwa shughuli za kawaida na mishahara. TZS 64,040,020.00 zilitumika kwa shughuli za maendeleo.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, katika kipindi cha Julai hadi Disemba, Wizara imetumia jumla ya TZS 16,821,942,476 ambapo TZS 14,751,942,476 kutoka kwa washirika wa maendeleo na TZS TZS 2,070,000,000 kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kati ya fedha zilizotoka kwa washirika wa maendeleo TZS 11,599,214,123 ni kutoka JICA kwa mchango 5 wa Soko la na Diko la Malindi, TZS 3,016,019,434 kutoka Benki ya Dunia kwa Mradi wa SWIOfish ambao tayari umemalizika na TZS 136,708,919 kutoka Shirika la IFAD kwa utekelezaji wa maendeleo ya Kilimo naUvuvi .

## 4.3 PROGRAMU YA AHUENI YA UVICO 19

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni moja kati ya taasisi zilipatiwa fedha za ahueni ya UVIKO 19. Kazi zilizopangwa kutekelezwa na Wizara katika programu hiyo ni ununuzi wa Boti 1077. Kati ya hizo Boti za Uvuvi 577 na boti za wakulima wa mwani 500, Ununuizi wa vifaa vya wakulima 5000 wa mwani; Ujenzi wa Mashamba100 ya kufugia vitango Bahari; Mashamba 60 yaKufugia Kaa, Mashamba 40 ya Kufugia Samaki, Ununuizi wa Mashine moja ya kutengeneza Chakula cha Samaki pamoja na utoaji wa mafunzo kwa wadau wa sekta ya Uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini.

Kati ya shilingi 28.8 Bilioni za sekta ya Uvuvi zilizowekwa benki ya CRDB, shilingi 5.9 Bilioni zilizowekwa kwa mradi wa Madagaa wa ZAFICO na kazi zifuatazo zimetumika.

a) Jumla ya shilingi 1.1 Bilioni zimetolewa kwa kampuni ya ZAFICO kutoka Benki yaCRDB ambapo shilingi 900 Milioni zimetumika.
b) Jumla ya majiko ya kisasa sitini (60) yenye thamani ya shilingi 126 Milioni kwa kaziya kukaushia dagaa yamenunuliwa kutoka China.
c) Chanja za kuanikia dagaa 2000 zimetengenezwa katika eneo la kama

Ujenzi wa kituo cha kutoa elimu kwa wajasiriamali wa dagaa kimekamilika katikaeneo la Kizimbani

Mafanikio yamepatikana katika ujenzi wa mashamba ya kufugia samaki, kaa na matango bahari. Jumla ya shilingi 4.47 Bilioni zilitengwa kwa kazi hiyo ambapo shilingi 2,059,542,800 bilioni zilitumika:

a) Kampuni ya Ezyfix imejenga jumla ya mabwawa hamsini na moja (51) kati ya mabwawa 100 ya ufugaji wa Matango bahari. Vilevile, kampuni hiyo imejenga mabwawa 30 kati ya mabwawa 60 ya ufugaji wa kaa.
b) Kampuni ya SENIC Construction LTD imejenga jumla ya mabwawa (15) kati ya mabwawa 20 ya ufugaji wa Samaki.
c) Wizara imepeleka jumla ya shilingi 2.5 Bilioni kwa Wizara ya Biashara na Viwanda kwa lengo la kuchangia ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu

mwani. Ujenzi wa Kiwanda unaendelea vizuri huko Chamanangwe Pemba.

d) Wizara imefunga mkataba wenye thamani ya shilingi 139,000 Milioni kwa ajili ya ununuzi wa mashine ya kutengezea chakula cha samaki. Bado mashine hiyo haijakabidhiwa kwa Wizara.

Jumla ya vifaa vya ukulima wa mwani vyenye thamani ya shilingi 1.58 Bilioni vimenunuliwa na kukabidhiwa Kampuni ya mwani ya Serikali (ZASCO) kwa kuwakabidhi wakulima 500 wa mwani.

Jumla ya shilingi 695 Milioni zilizotengwa kwa mafunzo ambapo shilingi 349 Milioni tayari zimetumika na mafanikio yafuatayo yamefikiwa:

a) Wadau 4000 wa sekta ya Uvuvi na wafugaji wa mazao ya baharini wamepatiwa elimu ya uhamasishaji wa mradi.
b) Mafunzo ya walimu wa walimu "Training of Trainers" yametolewa kwa watendaji hamsini (50) kuhusu matumizi ya kifaa cha kutafutia samaki "fish finder" na kifaa chenye kuonesha uwakilishi wa sehemu katika dunia (GPS).
c) Mafunzo kuhusu matumizi ya fish finder na GPS yametolewa kwa wanajamii 180 Unguja na Pemba.

Mafunzo ya Fish finder na GPS yamesaidia wavuvi kutoka Uvuvi wa uwindaji hadi Uvuvi wa maeneo maalum yenye Samaki. Hali hiyo inapunguza gharama za uendeshaji ikiwemo Mafuta, muda na mahitaji mengineyo.

## 4.4 MAMLAKA YA KUDHIBITI UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA (ZANZIBAR PETROLEUM (UPSTREAM) REGULATORY AUTHORITY)

Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) imeanzishwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia nambari 6 ya Mwaka 2016. Mamlaka hii imeanza kazi rasmi mwezi Machi 2017 kufuatia kuteuliwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji wa Mamlaka. Kwa mujibu wa Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, shughuli kuu ya Mamlaka ni

kusimamia na kudhibiti shughuli za Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

## CHANGAMOTO

1. Kujitokeza kwa waathiriwa wapya wanaodai fidia kila mara jambo linalozotesha jitihada za ulipaji fidia maeneo mbalimbali yalioathirika na zoezi la mitetemo.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kupitia ZPRA kuwashawishi na kuwapatia udhamini vijana wetu watakaosomea fani za mafuta na gesi ili kuwa na wataalamu wazawa watakaosimamia shughuli nzima ya mafuta na gesi kwa maslahi mapana ya nchi yetu.
2. Kamati inaitaka Wizara kupitia ZPRA kuzitangaza hatua walizozifikia za utafutaji wa mafuta hadi sasa ili kuwafanya wananchi kuwa na uelewa mzuri wa suala hilo na kuepukana na maswali ya mara kwa mara.
3. Wizara ihakikishe suala la ulipaji wa fidia kwa waathirika wa mtetemo wakati wa utafiti wa utafutaji wa mafuta linafanyiwa kazi haraka kutokana na ukweli kwamba suala hilo ni la muda mrefu sasa.
4. Kamati inaitaka Serikali kupitia ZPRA kuwa makini na kampuni zinazotaka kuja kuekeza kwenye suala la mafuta kwani uzoefu umeonesha kampuni nyingi zinazokuja kuleta maandiko yao hapa Zanzibar huwa hazna uwezo wa kifedha wa kufanya uwekezaji huo.

## 4.5 KAMPUNI YA MAENDELEO YA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA (ZANZIBAR PETROLEUM DEVELOPMENT COMPANY)

Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imeanzishwa chini ya kifungu cha 32 cha Sheria Nambari 6 ya Mwaka 2016 ya Mafuta na Gesi Asillia na kusajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni Sheria Nambari 15 ya Mwaka 2013. Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kampuni hiyo na kupokea taarifa ya utendaji wa shughuli zake.

## CHANGAMOTO

1. Kampuni ya mafuta ya ZPDC bado inajiendesha kwa kupokea ruzuku kutoka Serikalini.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaigiza Wizara kupitia kampuni ya ZPDC kuanza kufanya biashara ya kuuza mafuta ili iweze kuleta tija kwa serikali.
2. Kamati inaitaka Serikali izidishe umakini kwenye uanzishwaji wa vituo vya mafuta kwani baadhi yao vipo karibu na makaazi ya wananchi.

## 4.6 TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI ( ZAFIRI)

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini Zanzibar (ZAFIRI) ni Taasisi yenye jukumu la kupanga na kusimamia kazi zote za tafiti zinazohusiana na Uvuvi na mazao ya baharini pamoja na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wavuvi, wakulima wa mwani, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi imeanzishwa April 2019 chini ya hati ya Sheria (Legal Notice) namba 32 ya kifungu 53 cha Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984 na Kifungu 55 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Act No. 2 ya 2011 kwa madhumuni ya kuendeleza tafiti za Uvuvi na mazao ya baharini ili kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini.

## CHANGAMOTO

1. Taasisi toka ilipoanzishwa hadi kufikia sasa haina muundo wa kiutumishi.
2. Wavuvi wengi bado wanavua uvuvi wa kizamani wa kubahatisha bila ya kujua sehemu zinazopatikanwa kwa wingi samaki.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaiomba Wizara kupitia ZAFIRI kuharakisha upatikanaji wa muundo wa kiutumishi wa Taasisi hiyo
2. Kamati inaishauri Wizara kupitia ZAFIRI kuendeleza utafiti juu ya mambo ya bahari na kuhakikisha rasilimali za bahari zinaendelea kuwepo.
3. Kamati inaitaka Wizara kupitia ZAFIRI kuharakisha mpango wa kitalaamu uliokwenye majaribio wa mvuvi kueza kuelewa ni wapi kuna upatikanaji wa samaki kwa wingi kabla ya hata hajaenda kwenye shughuli za uvuvi.

## 4.7 IDARA YA MAENDELEO YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI

Idara ya maendeleo ya Uvuvi ina majukumu ya kuendeleza Uvuvi wenye tija na endelevu kwa kuhifadhi mazingira ya bahari Pamoja na rasilimali zake. Idara pia inawahudumia wavuvi, wafugaji wa samaki na mazao mengine ya baharini, wakulima wa mwani na wadau wengine tofauti wanaojishughulisha na mazao ya baharini.

**CHANGAMOTO**

1. Tatizo la wizi la mazao ya baharini haswa kwenye kilimo cha mwani.
2. Tozo ya kingilio kwenye maeneo ya hifadhi ya bahari ni kidogo sana ukilinganisha na tozo za wenzetu upande wa Tanzania bara.
3. Wavuvi wengi hawana ufahamu mzuri kwenye suala zima la faida za uhifadhi wa maeneo ya bahari.
4. Malighafi za utengezaji wa maboti zinazotoka nje ya nchi na kufanya zoezi la utengezaji wa boti kusuasua.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia idara ya uvuvi kuimarisha ulinzi kwenye maeneo yanayolimwa mwani kwa kuanzisha doria za ulinzi shirikishi zinazohusisha vijiji husika.

2. Kamati imegundua kuwepo kwa soko kubwa la samaki aina ya kambare kwa upande wa Tanzania bara na kwa kua Zanzibar inahifadhi kubwa ya samaki hao kamati inaitaka mamlaka kuanza kufanya biashara hiyo.
3. Kamati inaitaka idara ya uvuvi kurekebisha tozo za kuingia kwenye hifadhi kwa wageni kutoka dola tatu (3) za kimarekani ambayo ni tozo ya muda mrefu sana hadi kufikia dola 20 za kimarekani angalau ifanane na tozo ya upande ya Tanzania bara.
4. Kamati inaitaka idara pindi wavuvi wanapofanya makosa ya kuvunja sheria wanapaswa kupelekwa kwenye vyombo vya kutafsri sheia (Mahakama) ili wakahukumiwe na kuwataka walinzi wa vyombo vya dola kuacha kuwachukulia za kinidhamu wavuvi hao.
5. Kamati inaitaka Idara itumie nguvu nyingi kwenye zoezi la kutoa elimu ya uhifadhi wa bahari kwa wavuvi, kwani wavuvi wakipewa elimu watakua ni mabalozi kwa wengine.
6. Kamati inaitaka Wizara kupitia idara ya maendeleo ya uvuvi kuharakisha zoezi la kutengeneza boti kwani bado zoezi linakwenda kwa kasi ndogo.

## 4.8 KAMPUNI YA UVUVI (ZAFICO)

Kampuni ya Uvuvi (ZAFICO) ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa Sheria ya makampuni (Companies Act No. 15/20/13) ya mwaka 2017. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilianzisha Kampuni ya ZAFICO ikiwa ni katika kutekeleza Dira ya Maendeleo Zanzibar 2050, MKUZA III na Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025. Malengo makuu ya kuanzishwa kwa Kampuni hii ni pamoja na "Uvuvi endelevu wa kibiashara, kuimarisha miundombinu ya Uvuvi, kuanzisha viwanda, kuongeza ajira na pato la Taifa kwa kuzingatia malengo na mikakati ya muda mrefu ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kuimarisha Sekta ya Uvuvi nchini pamoja na kukuza Uchumi wa Buluu.

Kampuni ya Uvuvi imeundwa na wanahisa wanne ambao ni:-

i. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa hisa ya 45%

ii. Shirika la Biashara la Zanzibar (ZSTC) kwa hisa ya 27%

iii. Shirika la Bandari la Zanzibar (ZPC) kwa hisa ya 18%

iv. Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kwa hisa ya 10%

ZAFICO imeweza kubuni fursa ya miradi mikubwa minne ya biashara ambayo Kampuni itaweza kuwekeza. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

i. Uvuvi wa Bahari Kuu (Deep Sea Fishing)

ii. Kiwanda cha kusarifu minofu ya Samaki na vyumba vya baridi (An Integrated Processing and Cold Storage Facility)

iii. Kiwanda cha kusarifu Dagaa (Anchovy Processing Unit)

iv. Mradi wa ufugaji Samaki baharini (Cage Fish Culture)

## CHANGAMOTO

1. Wavuvi wengi hawana uelewa mzuri wa matumizi ya barafu za chengachenga.
2. Bado kampuni inajiendesha kwa ruzuku kutoka Serikalini.
3. Takwimu za idadi sahihi ya wavuvi haifahamiki.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara kupitia ZAFICO kuwapa elimu wavuvi juu ya umuhimu wa kutumia barafu ya chengachenga.
2. Kamati inaitaka wizara kupitia ZAFICO kushirikiana na taasisi ya Mtakwimu mkuu ili kuweza kujua idadi kamili ya wavuvi na samaki wanaopatikanwa katika bahari yetu.
3. Kamati inaitaka wizara kupitia ZAFICO kuja na mikakati itakayoonesha jinsi gani kampuni hiyo itajiendesha wenyewe bila ya kutegemea ruzuku kutoka serikalini na wao wawe sehemu ya kutoa gawio la kila mwaka (dividend) kwa Serikali.

4. Kamati inishauri ZAFICO kuwa na ubunifu na kuhakikisha inafanya kazi yenye kuleta tija.

## 4.9 DIKO LA SAMAKI MALINDI

Ujenzi wa Diko la samaki Malindi ni miongoni mwa ahadi alizoahidi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizowahidi wavuvi miongoni mwa vipaumbele vyake ni kuhakikisha wavuvi wanafanya kazi zao katika mazingira mazuri na rafiki kwa kazi zao.Jengo hilo linajengwa kwa Ushirikano baina serikali Japani na Serikali ya mapinduzi Zanzibar, Gharama za ujenzi wa Diko hilo la malindi ni Dola za kimarekani Milion 14, ambapo Serikali ya Japani inatoa dola za kimarekani milioni 13 na Serikali ya mapinduzi Zanzibar dola za kimarekani milioni 1,jengo hili linatarjiwa kuwa ni la ghorofa moja ,likiwa limegawika sehemu kuu mbili,sehemu moja ni Diko la meli na boti za uvuvi na sehemu ya pili itakua ni sehemu ya kuuzia samaki. Diko hili limeboreshwa Zaidi na kuwa na utofauti mkubwa na soko la zamani, Diko litakua na huduma zifuatazo:

1. Vibaraza sita tofauti vya kuendeshea minada mbalimbali ya samaki kwa wakati mmoja.
2. Vibaraza 150 vya kuuzia samaki kwa wauzaji wa kawaida
3. Diko hilo litakua na sehemu ya kuhifadhia samaki (Cold room) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 250 za samaki kwa wakati mmoja.
4. Diko hilo litakua na mgahawa wa kisasa na
5. Diko hilo litakua na sehemu ya maegesho ya magari.

## CHANGAMOTO

1. Ujenzi wa Diko kushindwa kukamilika kwa wakati.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara pindi Diko litakapokamilika wale wafanya biashara waliokua wakifanya biashara kupitia vibara vya zamani 43 wapewe kipaumbele kwanza kabla ya waombaji wapya.
2. Suala la usalama na afya za watumiaji wa diko hilo linapaswa kuzingatiwa na Wizara kwa kushurikiana na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji. Taratibu bora za uendeshaji wa shughuli za diko hilo zinapaswa kuwekwa ili kulinda afya za watumiaji wa huduma.
3. Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Baraza la manispaa katika kuhakikisha kuwa Diko na Soko la samaki Malindi linabakia na haiba yake kwa kufanya usafi wa kina katika eneo hilo.

### 4.9.1 KAMPUNI YA UGAVI WA GESI (GASCO) KINYEREZI

Kamati ya uchumi ya Baraza la wawakilishi ilipata fursa ya kutembelea Kampuni ya Ugavi wa gesi (GASCO) ambayo ni Kampuni Tanzu ya TPDC inayohusika na uendeshaji na ukarabati na ujenzi wa Miundombinu ya Taifa ya Gesi Asilia (NNGI).

Gesi inayochakatwa na kampuni ya Ugavi wa gesi (GASCO) hupokea gesi asilia kutoka vyanzo vikuu viwili ambavyo ni Madimba na Songo Songo katika Mikoa ya Mtwara na Lindi ambapo mabomba yanayosafirisha gesi yanatoka kwenye vyanzo hivyo hadi kituo cha mwisho cha kinyerezi.Bomba la gesi asilia linalotoka Madimba (Mtwara) hadi Tegeta (Dar es Salaam) lina Urefu wakilomita 551.Kampuni ya ugavi wa gesi ni kampuni inayoendeshwa na wazawa ambapo imeweza kuleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya nishati hapa nchini. Miongoni mwa mafanikio yaliopatikana kutokana na uwepo wa kampuni ya Ugavi wa Gesi (GASCO) ni kama zifuatazo:

1. Kuzalisha gesi ya umeme ambayo imeunganishwa kwenye kituo cha kufua umeme cha kinyerezi ambacho kimeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa.
2. Kuunganisha mfumo wa gesi ya kupikia majumbani ambapo kwa sasa baadhi ya maeneo ya Tanzania kwenye mikoa ya Lindi na Mtwara na baadhi ya maeneo ya

Dar es salam wameunganishwa na mfumo huo na kufungiwa mita zinazosoma matumiz ya gesi kama vile zinavyosoma mita za umeme za luku na Tukuza.

3. Kubadilisha mifumo ya magari kutoka utumiaji mafuta ya petrol na dizel na kuwa na mifumo inayotumia gesi kwenye mkoa wa Dar es salam.

**CHANGAMOTO**

1. Mahitaji ya ufungaji wa mifumo ya gesi kwenye gari yamekua makubwa lakini vituo vya kujazia gesi hizo mpaka kwa Dar es salam vipo viwili tu ambapo kimoja kipo Ubungo maziwa na chengine kipo Tazara.
2. Eneo la kupokea na kufua gesi hapo Kinyerezi limezungukwa na maakazi ya watu jambo ambalo ni hatari pindi ikitokea ajali.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaomba Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kupitia ZPDC kueka mikakati ya kushirikiana na TPDC ili Zanzibar nayo iweze kunufaika kwa kufungiwa mifumo ya kujazia gesi za kwenye magari kama wanavyonufaika wenzetu upande wa Tanzania bara.
2. Kamati inashauri wananchi waliovamia maeneo yanapotegemewa kuendeshwa kwa shughuli za mafuta na gesi kuacha kuendeleza shughuli za kibinaadam kwa usalama wa maisha yao na afya zao.

### 4.9.2 TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI (TAFIRI)

Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge namba 6 ya mwaka 1980 ili kukuza, kuendesha na kuratibu tafiti za uvuvi nchini Tanzania. Wazo la kuanzishwa kwa TAFIRI lilikuja baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1977. Kabla ya kuvunjika Jumuiya hiyo ilikuwa na kazi kadhaa, kati ya hizo ni pamoja na utafiti na maendeleo ya uvuvi.

Makao Makuu ya Taasisi yapo katika Jumba la Coelacanth House Kunduchi (Dar es Salaam). Taasisi hii inaundwa na Vituo vinne na Kituo Kidogo kimoja Ambavyo ni Kituo cha Mwanza na Kituo kidogo cha Sota kwenye Ziwa Victoria, Kituo cha Kigoma kwenye Ziwa Tanganyika, Kituo cha Kyela kwenye Ziwa Nyasa (Malawi) na Kituo cha Dar es Salaam kwenye Bahari ya Hindi. Kwa kua sheria hiyo ya awali ilishakua ya muda mrefu Serikali iliamua kuifuta sheria namba 6 ya 1980 na kuamua kutunga sheria nyengine inayojulikanwa kama sheria namba 14 ya mwaka 2016 ili taasisi hiyo kwenda na wakati.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati imefurahishwa na uhusiano mzuri uliopo baina ya Taasisi wa utafiti wa uvuvi na mazao ya baharini zote mbili yaani TAFIRI kwa upande wa Tanzania bara na ZAFIRI kwa upande wa Zanzibar na kuhimiza uhusiano huo uzidishwe Zaidi.
2. Kamati inaitaka Serikali kuiwezesha taasisi ya Utafiti ya Zanzibar yaani ZAFIRI kifedha kwani Tafiti nyingi zinazofanyika duniani, ZAFIRI hushindwa kushiriki kama Taasisi binafsi bali hufanya kazi hizo kupitia mgongo wa TAFIRI, hivyo mchango wa Zanzibar kwenye tafiti hizo hua haunokani.
3. Kwa kupitia ziara yake katika taasisi ya utafiti ya TAFIRI, Kamati imebaini kuwa shughuli za utafiti haziwezi kufanikiwa isipokuwa taasisi za utafiti ziwe na meli za kutosha na hivyo Kamati inaiomba Serikali kuongezea meli za kitafiti taasisi ya utafiti ZAFIRI ili iweze kufikia malengo yake.

### 4.9.3 MRADI WA TANLAPIA LTD BAGAMOYO

Tanlapia ni mradi mkubwa wa ufugaji samaki aina ya Sato (Tilapia) unaopatikana katika kijiji cha Nianjema wilaya ya Bagamoyo, katika Mkoa wa Pwani upande wa Tanzania bara.Mradi huu mpaka kumalizika kwake unategemwa kugharimu kiasi cha dola za kimarekani million 19 sawa na shilingi Bilioni 44.6 za kitanzania. Mpaka Kamati ilipoenda kulitembelea eneo hilo la mradi mnamo mwezi wa 8 (August), mradi ulikua

umeshatumia kiasi cha bilioni 11.6 za kitanzania, sambamba na hilo licha ya mradi kuwa unaendelea na hatua za ujenzi lakini pia wanaendeleza ufugaji wa samaki aina sato (tilapia) na pia wameanza kuuza samaki hao. Mradi huu utakapomalizika unategemewa kuwa ni mradi mkubwa Zaidi kusini mwa jangwa la sahara. Shamba la Tanlapia lina mkakati pia wa kuzalisha hadi vifaranga milioni 2 kupitia tecnologia ya kusafisha maji ambayo inasaidia uzalishaji wa samaki wengi katika eneo dogo ambapo itasaidia uvunaji wa tani elfu nane (8000) hadi elfu kumi (10000) kwa samaki za mwaka. Mahitaji ya samaki aina sato (Tilapia) hapa nchini ni makubwa sana kiasi kwamba soko lake ni la uhakika, soko kubwa la biashara hiyo lipo ndani ya nchi na pia wanasafirsha kwenda nchi za jirani. Kilo moja ya samaki aina sato (tilapia) huuzwa kati ya elfu saba( 7,000.00) hadi elfu nane (8,000.00) kwa shilingi za kitanzania.

### CHANGAMOTO

1. Chakula cha samaki wanaagiza kutoka nje ya nchi haswa kutoka nchi ya misri kutokana naTanzania bara kutokua na uwezo wa kuzalisha chakula hicho.
2. Changamoto ya vifaranga kuliwa na ndege waharibifu.
3. Miundo mbinu ya barabara sio rafiki hadi kufika eneo la mradi.

### MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Idara ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya baharini kuwahamasisha vijana wa kizanzibari kufanya ufugaji wa samaki wa maji baridi kwani samaki hao wanas oko la uhakika kwenye sekta ya utalii nchini.

## 4.9.5 HIFADHI ZA BAHARI NA MAENEO TENGEFU (MPRU)

Taasisi ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU), ilianzishwa kwa Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994, hii ni baada ya kubainika kuwa mazingira ya bahari yalikuwa hatarini kuharibika kabisa kutokana na uvuvi usio endelevu na matumizi mabaya ya rasilimali za bahari na fukwe nchini. Hifadhi ya bahari

ni chombo kinachohusika na uhifadhi na usimamizi wa rasilimali katika maeneo ya bahari kwa maendeleo endelevu kwa Tanzania Bara, Chini ya usimamizi wa Bodi ya Wadhamini wa Hifadhi za Bahari na MaeneoTengefu katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Kazi za hifadhi ya bahari na maeneo tengefu ni kama zifuatazo:

1. Kulinda na kuhifadhi maeneo yenye mkusanyiko mkubwa wa viumbe hai pamoja na mifumo ikolojia ya baharini na mwambao wa pwani.
2. Kusimamia maeneo ya Bahari na mwambao wa pwani ili kuwezesha matumizi endelevu ya rasilimali na ukarabati wa maeneo yaliyo haribiwa.
3. Kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi ndani ya Hifadhi wanashirikishwa katika nyanja zote za upangaji, uendelezaji na usimamizi wa Hifadhi na Maeneo Tengefu, wananufaika na kushirikishwa katika manufaa yatokanayo na Hifadhi na wanapewa kipaumbele katika matumizi ya rasilimali na fursa za kiuchumi zilizopo.
4. Ukuzaji wa elimu ya mazingira na usambazaji wa taarifa kuhusu uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali kwenye Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu.

## CHANGAMOTO

1. Kitengo kuwa chini ya Mkurugenzi wa Uvuvi na kuwa na Bodi iliyoteuliwa na Waziri jambo ambalo linalosababisha mkanganyiko katika maamuzi na usimamizi wa kitengo kutokuwa na mamlaka kamili ya kutekeleza majukumu ya kitengo na kutokuwa mamlaka hodhi (corporate body) inapelekea kitengo kushindwa kukopa kwa ajili ya kufanya shughuli za uwekezaji.
2. Sheria ya Hifadhi inakinzana na Sheria nyingine ikiwemo Sheria ya Ardhi, Sheria ya Misitu na Sheria nyingine.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri kutokana na uharibifu wa mazingira unavyozidi watu wakitaka kukata miti ya mikoko lazima kamati ya kijiji ihusishwe.

2. Kamati inashauri wizara ya uchumi wa bluu na uvuvi kupitia idara ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya bahari kuanzisha Tozo ya hifadhi ya bahari kwa wageni wote watakaoingia Zanzibar na iwe inakatwa kila anapoingia mgeni kupitia viwanja vya ndege na bandari za Zanzibar.
3. Kamati inapendekeza Wizara kupitia idara ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya bahari Zanzibar na kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuanzisha Leseni ya pamoja ya uvuvi ya jamhuri ya muungano wa Tanzania ambayo itakua inatumika pande zote mbili za muungano kuepuka mgogoro wanayokumbana nayo wavuvi mara kwa mara.

### 4.9.6 MAENDELEO YA KILIMO CHA MWANI

Kamati ya uchumi ya Baraza la wawakilishi inaipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inayongozwa na mheshimiwa Dr Hussein Ali Mwinyi kupitia wizara ya uchumi wa buluu na uvuvi Zanzibar kwa jitihada zake za kuliinua soko la mwani kisiwani Pemba kwa kuanzisha Kampuni ya biashara ya mwani inayoitwa ZASSCO. Kabla ya kuanzishwa kwa kampuni hii ya biashara ya mwani, wakulima wa zao hilo walikua wakinyonywa na wanunuzi wa biashara hiyo, ambapo bei ya juu kabisa ya zao la mwani ilikua ni shilingi mia sita (600) lakini baada ya kuanzishwa kwa kampuni ya mwani ya serikali bei ya zao la mwani lilibadilika na kufikia shilingi elfu moja (1000) za kitanzania. Kutokana na biashara ya zao la mwani kua soko zuri hivi sasa, kampuni mbalimbali za ununuzi zipatazo nane (8) zimejitokeza kutaka kununua zao la mwani kwa bei iliyopangwa na serikali.

### CHANGAMOTO

1. Mwani kukosa usafi kutokana na uwanikaji wake chini.
2. Kukosekana kwa soko la uhakika la moja kwa moja kwa wakulima wetu hasa kwa bidhaa zinazotokana na mwani ambazo zinazalishwa na vikundi vya usarifu.

3. Wakulima walio wengi ambao ni wanawake na wenye umri mkubwa kutokua na vifaa na zana na kushindwa kuogolea
4. Mabadiliko ya tabia ya nchi yanapelekea athari kwa ukulima wa mwanii
5. Migogoro kati ya wakulima wa mwani na sekta ya utalii haswa mahoteli
6. Wizi wa mwani kwa wakulima haswa baada ya bei kuongezeka
7. Mwani kukosa ubora kutokana na maradhi mbalimbali inayoukumba.
8. Kilimo cha mwani kinaathirika sana kutokana na uwepo wa migogoro iliopo baina ya wakulima wa mwani na wamiliki wa mahoteli.
9. Hakuna eneo maalum la kuwanikia mwani.
10. Boti zilizotengwa kwa ajili ya ukulima wa mwani, vijana wasiowaminifu wanazichukua na Kwenda kuvulia.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inashauri Wizara kwenye kuwawezesha vikundi vya wakulima wa mwani kuzingatia uwiano baina kisiwa cha Unguja na Pemba.
2. Kamati inaishauri Wizara kuwashajihisha vijana kwenye uzalishaji wa zao la mwani ambao kwa sasa una thamani kubwa. Utekelezaji wa jambo hilo ni ufanikishaji mzuri wa ilani ya chama cha mapinduzi kwenye kutimiza ahadi ya ajira laki tatu (300,000.00) kwa kupitia sekta ya mwani.
3. Kamati inashauri kuekwa ulinzi kwenye fukwe za bahari na maeneo yanayolimwa mwani kwani kumeanza kujitokeza tabia ya wizi wa mazao ya bahari haswa zao la mwani kutokana na kupanda kwake thamani.
4. Kamati inaishauri wizara kuwashajihisha vikundi vya wakulima wa mwani kwenda kujisajili rasmi ili vikundi hivyo viweze kukopesheka.
5. Kamati inaitaka wizara kwa kushirikiana na wizara ya Utalii, kuwaandalia wawekezaji maaeneo maalum kwenye maji mengi kwa ajili ya kufanya michezo ya bahari na kuwaacha wakulima wa mwani kwenye maji madogo.

6. Kamati inaitaka wizara kwa kushirikiana na wizara ya utalii kuwakumbusha wawekezaji kurudi kwenye mikataba yao ya kwamba fukwe si mali ya mtu na hivyo raia wote wapo huru kupita kwenye maeneo ya fukwe na hawapaswi kuzuliwa.

### 4.9.7 KIWANDA CHA MWANI (CHAMANANGWE)

Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika azma yake yake ya kuwainua wakulima wa zao la mwani ambao wamekua wakiteseka kwa muda mrefu kutokana na soko la biashara hiyo kua duni, itakumbukwa ya kambwa miongoni mwa ahadi alizozitoa Mheshimiwa Rais ni kuwainua wakulima wa zao hilo la mwani, alipoingia madarakani tu hakusahau ahadi yake na mara moja tu eneo la kujengwa kiwanda cha mwani lilitengwa na ilipofika tarehe 24/06/2022 mkataba wa ujenzi baina Wizara ya Biashara na kampuni ya ujenzi ya KMKM Construction ulifungwa ambapo ujenzi huo ni wa mwaka mmoja, Ujenzi wa kiwanda hicho hadi kumalizika kwake, unategemewa kugharimu kiasi cha Bilion 8.2. Eneo lote la kiwanda linaukubwa wa hekari Tano, Kiwanda kitakapomalizika litakua na uwezo wa kuhifadhi tani elfu thelathini (30) kwa wakati mmoja, jengo hilo litakapomalizika litakua na Ghala (warehouse), Ofisi pamoja maabara za kuchakata mwani.

### CHANGAMOTO

1. Umeme ni mdogo sana kisiwani Pemba,hali ambayo inategemewa kuja kudhorotesha utendakazi wa shughuli za kiwanda hicho.
2. Uzalishaji mdogo wa zao la mwani nchini ni suala la kuangaliwa kwa kina kwani uwezo wa wazalishaji wetu kwa sasa ni tani 11,000 tu ingawa mahitaji yetu kwa ajili ya kiwanda ni tani 30,000.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kulifikiria suala la nishati ya umeme kisiwani Pemba kwani kwa sasa fursa za uwekezaji kisiwani Pemba zimeanza kufunguka hivyo suala la umeme likiwa ni kikwazo suala la uwekezaji litakuja kuathirika.
2. Serikali, kupitia Wizara ya uchumi wa buluu na Uvuvi kwa kushirikiana na Wizara inayohusika na Kilimo iandae mpango maalum wa kuinua kiwango cha uzalishaji wa zao la mwani nchini ili kuhakikisha mahitaji ya malighafi kwa kiwanda chetu yanatimia.
3. Kamati inashauri Wizara kuwa na mikakati madhubuti ya kuongeza uzalishaji wa mwani nchini ili kukidhi mahitaji ya kiwanda.
4. Wizara ivipatiye vikundi vya uzalishaji wa mwani mashine za kusarifu mwani ili kuongeza thamani ya zao hilo na kuleta tija kwa wazalishaji.

## 4.9.8 ENEO LA USARIFU NA UANIKAJI DAGAA NDAGONI

Kwa mujibu wa historia eneo la Ndagoni ndio eneo la mwanzo kwa Zanzibar kuanza kwa shughuli za ujasiriamali wa kusarifu na kuanika dagaa. Eneo hilo lina ukubwa wa ekari tatu (3), eneo hilo limechaguliwa na serikali kujengwa kiwanda kikubwa kwa ajili ya kuja kuanikia na kusarifia dagaaa, lakini hadi sasa ujenzi huo huo bado haujaanza. Kiwanda hicho kitakapokamilika kinategemewa kuinua soko la biashara ya dagaa nchini kwani kwa sasa soko la biashara hiyo lipo ndani ya Zanzibar na baadhi ya nchi jirani za Tanzania bara, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na Malawi. Pindi kiwanda hiki kitakapojenga ni mategemeo ya kamati biashara hiyo itaingizwa kwenye soko la ushindani la dunia na hivyo kupelekea kuinua uchumi wa Zanzibar na wajasiriamali wa biashara hiyo.

## CHANGAMOTO

1. Eneo linalotegemewa kujengwa kiwanda hadi sasa halina hati miliki jambo linalopelekea kushindwa kuanza kwa ujenzi wa kiwanda hicho.

2. Wananchi wanaozunguka eneo hilo hadi sasa wamezuiwa kufanya shughuli yoyote lakini pia hawajalipwa fidia kutokana na vipando vyao vilivyopo eneo hilo.
3. Dagaa linaanikwa chini hivyo kuifanya bidhaa hiyo kushuka thamani kutokana na kuchanganyika na mchanga.
4. Wasajisiriamali hao hawana miundombinu ya kuhifadhia dagaa, pindi mvua inaponyesha dagaa lote huharibika.
5. Tatizo la uchimbwaji wa mchanga unaochimbwa na mwananchi mmoja wa eneo hilo jambo ambalo linasababisha kuwepo kwa mashimo na kujaa maji maeno hayo.

**MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI**

1. Kamati inaitaka Wizara kupitia Idara ya uvuvi na mazao ya baharini pamoja na Afisi kuu Pemba kulitafutia ufumbuzi suala la fidia mapema kwani kadri muda wa kulipa fidia unavyochelewa unasababisha thamani ya fedha nayo kushuka.
2. Kamati inaitaka wizara kupitia idara ya uvuvi na mazao ya baharini pamoja na Afisi kuu Pemba kulifanyia haraka suala la kulitafutia hati miliki eneo hilo ili ujenzi uanze, kwani bila ya kupatikana kwa hati miliki, ujenzi wa kiwanda hicho hautoanza.
3. Kamati inataka wizara kupitia Afisi kuu pemba kuwachukulia hatua watu wanaofanya uharibifu wa mazingira kwa kuchimba mchanga eneo hilo.

### 4.9.9 WAKULIMA WA MWANI WA JIMBO LA KOJANI (CHWALE)

Kilimo cha mwani ni moja ya kilimo kilichopewa kipaumbele kikubwa sana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hali ambayo imewapa motisha ya hali ya juu kabisa wakulima wa zao hilo kujikita kwenye kilimo hicho licha ya changamoto mbalimbali zinazolikumba zao hilo. Zao la mwani limekua na thamani kubwa sana kutokana na kuwa na matumizi mbalimbali kama vile chakula katika nchi za mashariki ya mbali (Bara la Asia), pia mwani

ulosagwa unatumika kutengenezea manukato, marashi pamoja na sabuni. Zanzibar ni nchi ya nne (4) kati ya nchi zinazozalisha mwani mwekundu ikiongozwa na Indonesia, Ufilipino na Malaysia. Pamoja na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali katika kuliinua soko la mwani ni ukweli usiopingika kuwa kwa muda mrefu sasa bei ya mwani imekua na changamoto ukilinganisha na maeneo mengine wanayolima zao hilo. Kutokana na changamoto zinajitokeza mara kwa mara kwa wakulima wa zao la mwani pamoja na mambo mengineyo Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi Zanziabr ilifanikiwa kufika katika kijiji cha Chwale katika jimbo la Kojani na kukutana na vikundi mbalimbali vinavyolima zao la mwani kwa lengo la kuwasikiliza kero zao na baadae kuzitafutia ufumbuzi

## CHANGAMOTO

1. Umbali wa maeneo wanapoendesha shughuli za kilimo na makazi yao jambo ambalo linapelekea kushindwa kudhibiti ulinzi mzuri wa mashamba yao hali inayopelekea kuibiwa kwa mwani wao.
2. Ukosefu wa vifaa vya kuanikia na kuhifadhia mwani ikiwemo na kamba.
3. Wana ukosefu wa viatu vya kuendea baharini.
4. Idadi ya wanavikundi ni kubwa ukilinganisha na boti walizonazo.
5. Mvutano baina ya wakulima wa mwani na wavuvi.
6. Kilimo cha mwani kinazorota kutokana na uwepo wa upungufu mkubwa wa maboya ya kufungia kamba za mwani.
7. Vikundi vya ukulima wa mwani vipo vingi, ila vingi vya vikundi hivyo hawana elimu ya kusajili vikundi hali inayopelekea kushindwa kukubalika na mabenki na hatimae kukosa fursa za uwezeshwaji.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka wizara ya uchumi wa buluu na uvuvi kuwawezesha wanavikundi hao usafiri hata wa maringi mawili kwa njia ya mkopo ili kuweza kutatua changamoto ya usafiri.

2. Kamati inaitaka wizara kuwawezesha wanavikundi hao vifaa vinavyohusika na mpango wote wa kilimo cha mwani ikiwepo kamba za kuanikia mwani na viatu vya kuendea baharini pamoja na maboya ya kuogelea ili kuifanya shughuli iyo kuwa nyepesi.
3. Kamati inaitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na uvuvi kupitia idara ya uvuvi na mazao ya baharini kutafuta muafaka wa migogoro inayoendelea baina ya wakulima wa mwani na wavuvi hususan katika kisiwa cha Kojani.
4. Kamati inaiomba Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Idara ya uvuvi na mazao ya baharini kuendelea na zoezi la kutoa elimu kwa vikundi juu ya umuhimu wa kujisajili kwani kushindwa kufanya hivyo kutapelekea kukosa fursa mbalimbali ikiwemo fursa ya kukopeshwa na kuwezeshwa.

### 4.9.9.1 ENEO LA VIWANDA LA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

Ni eneo la fungu refu lililopo Mkokotoni lililotengwa na Serikali kwa ajili ya ujenzi wa:

- Kiwanda cha kuchakata samaki
- Kiwanda cha kutengeneza chakula cha samaki
- Kiwanda cha kutengeneza boti.

Wizara iliingia mkataba na Kampuni ya Khayru ya nchini Sri Lanka wa kuliendeleza eneo hilo kwa mujibu wa mpango wa matumizi uliopangwa. Kwa bahati mbaya mkataba huo haujaweza kufanyiwa kazi hadi Kamati ilipolitembelea eneo hilo kutokana na mtikisiko wa kuichumi unaoikumba nchi ya Sri Lanka uliopelekea kupoteza mwelekeo kwa makampuni mengi ya nchi hiyo na kuathiri pia malengo ya kampuni yetu mpya iliyoanishwa chini ya mkataba huo ijulikanayo kama ZAFICO KHAYRU.

Kutokana na kuzorota kwa mradi huo chini ya ZAFICO KHAYRU, Wizara inalenga kulitumia eneo hilo kwa utekelezaji wa mradi wa IFAD ambapo kwa upande wa Zanzibar jumla ya dola milioni 8 zinatarajiwa kutumika.

## CHANGAMOTO

1. Mradi unakabiliwa na changamoto ya kutoanza utekelezaji kwa muda mrefu
2. Ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaomiliki sehemu ya eneo la mradi unaosababishwa na taratibu za ulipaji zinazosimamiwa na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kwa kuzingatia kuwa sehemu ya eneo lililokusudiwa kutekelezwa miradi ya viwanda vya uchumi wa buluu inamilikiwa na wananchi, Kamati inaitaka Wizara kwa kushirikiana na Afisi ya Rais, Fedha na Mipango, kufanya juhudi za makusudi za kuwalipa fidia wamiliki wa eneo hilo ili weweze kutafuta maeneo mengine kwa ajili ya shughuli za maendeleo.
2. Kutokana na changamoto zilizoikumba Kampuni ya Khayru ambayo ndiyo mshirika wa Kampuni ya ZAFICO katika utekelezaji wa miradi hii, Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuangalia uwezekano wa kuvunja mkataba huo.

## 4.9.9.2 UFUGAJI WA MATANGO (MAJONGOO) BAHARI - UKUNJWI

Ufugaji wa matango (majongo) bahari hivi sasa umekua na tija kubwa kutokana na umuhimu wake katika soko la dunia. Bei ya matango bahari sokoni inazidi kuwapa hamasa wafugaji ambapo kilo moja inauzwa hadi shilingi 300,000 za kitanzania. kutokana na hali hiyo, wananchi mbalimbali wameanza kujitokeza kufanya shughuli hiyo. Kwa upande wa wananchi wa kijiji cha Ukunjwi, walianza ufugaji wa matango bahari  hata kabla bidhaa hiyo haijapanda bei, na kwa kuwa lengo la Serikali ni kuwawezesha wananchi wengi kwa ujumla na si mtu mmoja mmoja, ilipofika 2021 wananchi wa kijiji cha Ukunjwi walilazimika kujikusanya kwa umoja wao na kuamua kuanzisha kikundi kinachoitwa NIA ZETU kinachojishughulisha na ukulima wa matango bahari wakiendesha shughuli hizo kwa kutumia bwawa lililojengwa kienyeji hali ambayo inasababisha kutofikia malengo waliyojiekea. Kwa kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na

Uvuvi kwa kupitia idara ya uvuvi na mazao ya baharini inaendelea na mpango wa kujenga mabwawa ya matangao bahari yapatayo mia moja (100) kwa mgawanyo wa kisiwa cha Pemba mabwawa hamsini (50) na Kisiwa cha Unguja mabwawa hamsini (50), kijiji cha Ukunjwi tayari kimeshajengewa mabwawa matano kama mfano (pilot area) kwa maeneo mengine ambayo yanategemewa kujengewa kwa njia ya mkopo.

## CHANGAMOTO

1. Kikundi hakina utaalamu kukausha matango (majongoo) bahari hali inayopelekea kupungua kwa ubora na kushuka kwa thamani.
2. Kikundi kina changamoto ya kupata vifaranga.
3. Taratibu za mikopo baina Wizara na Benki ya CRDB hazijakamilika hali inayopelekea kuchelewa kukabidhiwa kwa mabwawa kwa wananchi hao.
4. Wizi wa matango bahari kabla ya muda wa kuvunwa na wenye mashamba unarejesha nyuma juhudi za wafugaji hao.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Idara ya Uvuvi na mazao ya baharini kulitafutia ufumbuzi suala la upatikanaji wa uhakika wa vifaranga vya matango bahari na kuandaa mpango mzuri wakuvigawa kwa wafugaji.
2. Kamati inaitaka wizara kulifanikisha suala la ufungaji wa mikataba baina ya serikali na benki ya CRDB ili wananchi wanaohitaji kukopeshwa wapawe ili waweze kuyaendesha maeneo hayo ili waweze kujikwamua kimaisha.
3. Kwa kuwa ufugaji wa matango bahari unahitaji taaluma, Kamati inaiomba Wizara kuwapatia wafugaji hao taaluma ya ufugaji bora ili wapate matango bahari yatakayokuwa na kiwango kizuri na kupata bei nzuri sokoni.

#### 4.9.9.3 KIWANDA CHA KUKAUSHIA DAGAA – KAMA

Kiwanda kinategemewa kujengwa katika eneo la Kama ambapo jumla ya hekta 17 zimetengwa kwa ajili ya shughuli za wajasiriamali wanaoshughulikia sekta ya dagaa. Kiwanda hicho kinatarajiwa kutumia kwa kiasi kikubwa malighafi ya dagaa linalozalishwa nchini. Katika kuhakikisha kiwanda kinapata malighafi ya kutosha, Wizara imeanza mchakato wa kuwainua wajasiriamali wa dagaa na kuwafanya waweze kuzalisha dagaa lenye kiwango cha juu. Wizara imedhamiria kuwa na sehemu ya majiko ya kisasa ya kuchemshia dagaa pamoja na chanja za kisasa za kukaushia. Jumla ya chanja 2070 zimetengenezwa kwa ajili ya kuanikia dagaa na majiko 60 ya kuchemshia yameingia nchini. Vifaa hivyo vitagawiwa kwa wananchi kwa utaratibu maalum ulioandaliwa ili kuvifanya viwe endelevu. Lengo kuu la kuanzisha shughuli hizi ni kuzalisha dagaa bora litakalouzwa kwenye soko la ndani na nje ya nchi. Mara baada ya kukamilika kwa mradi huu, mfumo mzima wa biashara ya dagaa nchini utabadilika na kuondokana na hali ya sasa ya kuuza dagaa kinyemela na kumnufaisha dalali na mnunuzi na kumuacha mvuvi akiwa na hali duni ya kiuchumi.

#### CHANGAMOTO

1. Hadi wakati Kamati ilipofanya ziara, Wajasiriamali wa sekta ya dagaa bado wana hali ngumu ya kiuchumi kutokana na kukosa thamani ya kazi yao.
2. Baadhi ya wananchi kuhodhi eneo ambalo lingepaswa litumike kwa maendeleo ya sekta ya dagaa nchini ni jambo linalokwaza uendelezaji wa shughuli za dagaa.
3. Ukosefu wa soko la uhakika kwa wajasiriamali wa dagaa mara baada ya kukamilisha shughuli za uzalishaji.
4. Uchache wa vifaa vya kuchemshia na kuanikia dagaa kulingana na mahitaji ya wajasiriamali wanaojihusisha na sekta hiyo.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara kutekeleza kivitendo mipango yake ya kuanzisha kiwanda cha dagaa na kuongeza thamani ya zao hilo na kuwainua wajasiriamali waliojikita kwenye sekta hiyo.
2. Ni wajibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuhakikisha kuwa inamiliki eneo la kimkakati kwa ajili ya uendelezaji wa sekta ya biashara ya dagaa likiwemo eneo la mlango wa bahari kwa ajili ya kurahisisha usafirishaji wa bidhaa hizo.
3. Ili kupata uhakika wa dagaa la kutosha kwa ajili ya malighafi ya kiwanda, Kamati inashauri Wizara kushirikiana na Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kuwapatia mikopo nafuu wajasiriamali wanaojishughulisha na sekta na kuongeza kiwango cha uzalishaji.

## 4.9.9.4 MASHAMBAA YA UFUGAJI WA KAA KISIWANI PEMBA

Wakati wa mripuko wa janga la uviko 19, shughuli nyingi za kiuchumi ziliathirika hususan shughuli za uvuvi na ufugaji wa mazao mbali mbali ya baharini. Serikali kwa kupitia mradi ya Uviko 19 iliamua kuwawezesha vijana kwenye sekta hii pale ilipoamua kuanzisha programu maalum za mashamba ya ufugaji wa Kaa, ambapo hadi sasa jumla ya mashamba sitini (60) yameanzishwa nchini. Kati ya mashamba hayo, jumla ya mashamba 12 yamejengwa katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na 18 yamejengwa katika Mkoa wa Kusini Pemba na mashamba 30 yaliyobakia yamejengwa Unguja. Uzalishaji wa Kaa kwa mwaka unatarajiwa kua ni Zaidi ya tani 360. Mashamba hayo yanatolewa kwa njia ya mkopo ambapo wananchi waliopatiwa mikopo hiyo wanapaswa kurejesha kidogokidogo gharama za mkopo huo. Gharama za kujenga mabwawa hayo hadi kukamilika kwake ni jumla ya shilingi 4,000,000 milioni kwa bwawa moja ambapo gharama hizo zinahusisha ujenzi wa uzio wa bwawa hilo pamoja na vifaranga vya kaa 1240.

## CHANGAMOTO

1. Uzio wa mashamba hayo ya Kaa ni mwepesi na mdogo sana, maji yakijaa Kaa wanatoka nje na hawarudi kwenye mashamba.
2. Kupanda na kushuka kwa bei ya kaa sokoni ni jambo linalowarejesha nyuma wafugaji wetu kwani wakati mwengine wafugaji hununua vifaranga kwa bei ya juu lakini wanapofika muda wa mavuno hupata bei ndogo sokoni.
3. Suala la wizi kwenye mashamba ya kaa bado ni kubwa sana hali inayowarejesha nyuma wafugaji.
4. Zanzibar kama Nchi haina mamlaka ya kutuma mazao kwa kuyauza hadi wapate uthibitisho kutoka wizara ya uvuvi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
5. Vikundi vingi walivyowezeshwa kwa kupatiwa mashamba ya ufugaji wa Kaa havina uelewa wa kwamba, miradi hiyo ni mikopo inayopaswa kurejeshwa kidogokidogo.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kuendelea kuwapatia wafugaji elimu juu shughuli za ufugaji wa Kaa.
2. Kamati inaishauri Wizara kulifikiria suala walilolamikia wafugaji wa kaa kua uzio ni mdogo na kulitafutia ufumbuzi unaostahiki.
3. Ni wajibu wa Wizara kuanzisha programu ya kuwapeleka wanavikundi kwenye vikundi vilivyofanya vizuri ili wapate fursa ya kujifunza kwa vikundi vyengine.
4. Kamati inaitaka Wizara, ifikirie namna ya kuwaongezea mabwawa wanavikundi kwani idadi ya wanavikundi ni kubwa kuliko uwezo wa mabwawa yao na hivyo wanavikundi hao kupoteza nguvu nyingi bila ya kupata maslahi ya kiuchumi.

#### 4.9.9.5 MRADI JUMUISHI WA UWEZESHAJI WANAWAKE KATIKA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI.

Wanawake wanapitia changamoto mbalimbali na kwa kipindi kirefu hawakuwa wakihusishwa na shughuli za uzalishaji mali ambapo shughuli yao kubwa ilikuwa ni kufanya kazi za nyumbani tu hali iliyowafanya kuwa ni tegemezi.

Awamu zote zilizopita za Serikali zilikua na utaratibu wa kuwainua kina mama kwa njia moja au nyengine. Serikali ya awamu ya nane (8) kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na kwa kushirikiana na wadau wengine iliandaa miradi mbali mbali kwa madhumuni ya kuwawezesha na kuwafanya wanawake waweze kujikwamu na wimbi la umasikini ambalo limeshamiri kwenye nchi zetu za Afrika. Miongoni mwa miiradi ambayo inasimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kama ifuatayo:

1. Mradi wa Ahueni ya Uviko 19, ambayo hadi sasa imeweza kutoa mikopo na kuwanufaisha wanawake 773.
2. Mradi wa kuendeleza Uchumi wa Buluu katika eneo la Bahari ya Tanga pemba (Tanga-Pemba Seascape). Mradi huu upo chini ya ubalozi wa Ireland nchini Tanzania ambapo lengo lake ni kuwawezesha wanawake wanaojishughulisha na shughuli zinazoshabihiana na uchumi wa buluu, na hadi kufikia sasa wamefanikiwa kuwawezesha wanawake 60 kwa kupitia vikundi mbalimbali.
3. Wizara ya biashara na maendeleo ya viwanda kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na EIF waliviwezesha vikundi vya kina mama kwa kuwapa boti 8 za Fibre kwa ajili ya ukulima wa mwani na hadi sasa wanawake walionufaika na mradi huo ni 134.
4. Jumuia ya Zanzibar Maisha Bora Foundation inayoongozwa na mke wa Rais wa Zanzibar Mama Maryam Mwinyi, iliwawezesha kina mama 241 kupitia vikundi 11 vya shughuli za uchumi wa buluu kwa kuwapa boti 8 za fiber zenye uwezo wa 15HP.

## CHANGAMOTO

1. Gharama za usafirishaji wa boti haswa zilizotengenezwa nje ya Zanzibar ni kubwa sana, na wizara hua haina bajeti kwa ajili ya usafirishaaji, jambo ambalo mzigo huo hubebwa na wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.
2. Eneo la Wizara la kuhifadhia boti zilizokwisha kutengenezwa ni dogo na halikidhi mahitaji halisi ya shughuli hiyo.
3. Miradi ya utengenezaji boti ilichelewa kutokana na ukosefu wa mashine za boti za Mwani ambapo zinahitaji uwezo wa mashine wa HP 9.9
4. Benki ya CRDB imekua sehemu ya tatizo kwenye utekelezaji wa shughuli hizi za uwezeshaji kwani licha Wizara kukubaliana na CRDB kupunguzaa vikwazo kama inavyofanya kwa mikopo yao ya kawaida bado wanaendelea na utaratibu wao uleule jambo linalowakatisha tamaa wananchi.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara ifuatiliye kwa karibu sana zoezi la ujazaji wa mikataba ya mikopo ya boti na kwa kushirikiana na wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya wasimamiye marejesho ya mikopo hiyo ili kuwapatia wananchi wengine wanaohitaji.
2. Wizara ya Uchumi wa buluu na Uvuvi ikae na Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuondoa vikwazo vya kodi vinavyojitokeza wakati wa usafirishaji wa boti.

## 4.9.9.6 SONGORO MARINE TRANSPORT

Ni kampuni ya Kizalendo ya utengenezaji wa boti ambayo Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeingia mikataba nayo kwa ajili ya utengenezaji wa boti 73 za mita saba na boti 75 za mita nane kupitia fedha za ahueni ya UVIKO 19. Hadi wakati wa ziara hii, Kampuni imeshakabidhi Wizarani jumla ya boti 15 za mita saba na tayari boti nyengine 20 za mita saba zimekamilika tayari kwa kukabidhiwa na kufanya jumla ya boti 35 zilizotengenezwa. Aidha, boti 38 zilizobakia zinatarajiwa kujengwa ndani ya mwezi wa Septemba 2022.

Kwa upande wa boti za mita 8, ujenzi wa boti ya awali unakaribia kukamilika ambapo mazoezi ya baharini yatafanyika kabla ya kutengeneza boti nyengine za aina hiyo, ilikubaini kasoro zilizopo mapema na kurekebisha kwenye utengenezaji wa boti zinazofuata. Ujenzi wa boti 75 za aina hii unategemea kukamilika mwishoni mwa mwezi wa Oktoba, 2022.

Mara baada ya kukamilika kwa boti hizo, zitakabidhiwa kwa wavuvi ikiwa ni seti nzima inayojumuisha boti yenyewe, fish finder, GPS, mitego ya samaki.

## CHANGAMOTO

1. Uchelewaji wa malighafi za ujenzi wa boti ambazo huagizwa kutoka nje ya nchi na kupelekea kuchelewa kwa kazi.
2. Uchelewaji wa malipo ya awamu ya kwanza ya boti 15 zilizokabidhiwa kwa takriban miezi miwili kutoka benki ya CRDB, Jambo ambalo lilikwaza maendeleo ya kazi.
3. Benki ya CRDB ambayo ndiyo iliyoingia mkataba na Wizara kwa ajili ya utoaji wa fedha za mradi huu haina mpango mzuri wa utoaji wa fedha. Mara baada ya uwasilishaji wa mahitaji ya malipo ya awamu ya kwanza, Benki ilitoa matakwa mengine bila ya kuzingatia muda wa kukamilika kwa mradi huu.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Wizara iendelee na kazi ya uhamasishaji wa wananchi ili waitumiye ipasavyo fursa ya miradi iliyopo kwa ajili ya kujikwamua kiuchumi na kuongeza pato la Taifa letu.
2. Wizara ifanye ushindani wa mabenki katika shughuli za utoaji wa mikopo ili kuongeza ufanisi katika huduma hiyo na kufanikisha miradi iliyopangwa kwa wakati.
3. Kampuni za kizalendo zinapaswa kupewa kipaumbele kwenye tenda za kazi za Wizara kwani zinaonesha kufanya vizuri kwenye majukumu yao.

4. Kampuni ya Songoro Marine Transport imeshauriwa kufungua tawi lake Zanzibar ili kuwapa fursa ya ajira vijana wetu.
5. Wizara ikae na Wizara nyengine ili kutatua changamoto ya usafirishaji wa boti kutoka Tanzania Bara.

### 4.9.9.7 SOKO LA SAMAKI – FERI

Ni miongoni mwa masoko ya zamani jijini Dar-es-salaam lililoanzishwa mwaka 1950 kwa ajili ya kupokea samaki kutoka kwa wavuvi na lilikua kwenye mazingira duni kwa kukosa miundombinu ya maji, umeme na huduma ya choo. Soko hilo lilijengwa upya mnamo mwaka 1999 kwa gharama ya jumla ya shilingi Bilioni 12.26 ikiwa ni msaada kutoka Serikali ya Japan, kati ya hizo shilingi 260 ni mchango wa Halmashauri ya Jiji la Dar-es-salaam na kufunguliwa rasmi mwaka 2002.

Lengo kuu la kuanzishwa kwa soko hilo ni kuongeza ajira kwa wanajamii, kuimarisha usambazaji wa samaki, kuimarisha afya ya jamii pamoja na kuinua pato la wananchi na Taifa kwa ujumla kupitia shughuli za kiuchumi zilizopo sokoni hapo. Uendeshaji wa soko uko chini ya bodi na limetoa ajira kwa Zaidi ya watu 3000. Kamati ya Uchumi ya Baraza la Wawakilishi ilipata fursa ya kulitembelea soko hilo na kujionea shughuli za kiuchumi zinavyoendeshwa sokoni hapo.

Kufuatia ziara hiyo, Kamati imebaini kuwa Utaratibu wa Zanzibar wa kusimamia kikamilifu suala la kujiepusha na uvuvi haramu umesaidia sana kulinda mazingira na kuipa heshima nchi yetu mbele ya jamii ya wavuvi.

### CHANGAMOTO

1. Wingi wa wafanyabiashara kuliko uwezo wa soko unaopelekea miundombinu ya soko kuharibika mara kwa mara. Soko hilo limejengwa kwa ajili ya wafanyabiashara 1500 lakini kiuhalisia soko lina wafanyabiashara 3000 kwa sasa.

2. Kujaa kwa mchanga kwenye maeneo ya kuegeshea boti za uvuvi kunakosababisha boti zishindwe kuegeshwa.

## MAONI, USHAURI NA MAAGIZO YA KAMATI

1. Uendeshaji wa masoko yetu makubwa hapa Zanzibar likiwemo soko la Malindi ni vyema ukafuata mfumo wa soko la feri ambao unadhibiti makusanyo na kutatua changamoto za wafanyabiashara bila ya usumbufu.
2. Wizara izingatiye suala zima la kuweka vituo vya huduma ya kwanza kwenye masoko yetu makubwa kwa ajili ya kuwasaidia wafanyabiashara wanapofikwa na dharura za kiafya kabla ya kuwapeleka hospitali kwa matibabu zaidi.
3. Ili kuyatunza masoko yetu, ni vyema Wizara ikawa na ubunifu wa miradi tofauti kwa wananchi na kupunguza idadi ya wafanyabiashara masokoni.
4. Usafi ni jambo la msingi kwa masoko yetu ili kulinda afya za wafanyabiashara na walaji ikizingatiwa kuwa masoko hayo yanauza samaki ambao ni kitoweo kikuu kwa watu wengi nchini.
5. Wizara isichoke kuendelea na usimamizi wa maeneo ya hifadhi na kuhakikisha uvuvi unaofanyika hapo ni ule unaokubalika kisheria. Utekelezaji wa suala hili bado haujakubalika kwa wavuvi wetu na hivyo ni busara Wizara ikaendelea na programu za kuwaelimisha juu ya umuhimu wa jambo hili.
6. Kamati inashauri waendeshaji wa soko na Diko la Samaki Malindi wapatiwe fursa ya kujifunza namna bora ya uendeshaji wa soko kwa wenzao wa soko la feri.

## SEHEMU YA TANO

## 5. HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar na Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020, Kamati ya Uchumi imetoa maoni, ushauri na mapendekezo kadhaa kwa Taasisi inayozisimamia ikiwa ni

- Afisi ya Rais, Fedha na Mipango,
- Afisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji na
- Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

Ni matumaini ya Kamati kuwa, maoni, ushauri na maagizo yaliyotolewa kwa Taasisi hizo yatasaidia katika kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, kuongeza uwajibikaji kwa viongozi na wanaoongozwa, kuongeza pato la Taifa na kusukuma gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Mwisho, Kamati inatoa shukurani za dhati kwa Uongozi wa Baraza la wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa ulioiwezesha kufanya shughuli zake kwa ufanisi na kuandaa ripoti kama inavyostahili.